

**Taraji** kuwa msema chochote BET

UKURASA 20





**Man** United haina mpango na Ramos

UKURASA 21

**MAISHA**

Nipashe Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



Furahia chachandu ya pilipili



MAISHA NI NYUMBA
Namna ya kuchagua fimbo za chuma za kuwekea pazia



HARUSI



NYWELE FUPI
Urembo wenye faida nyingi kwa mwanamke

UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 20, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580617

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




RIPOTI MPYA

# Mapenzi chanzo ajali za barabarani

• **Polisi** wasisitiza ni sehemu ya mzizi wa vifo 460 *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 5

**KAMERA KUKABILI UHALIFU DODOMA**

UONGOZI wa Mkoa wa Dodoma umesema kamera za usalama zitafungwa katika maeneo...

UKURASA WA 5

**KONDAKTA AUAWA KWA JIWE AKIGOMBEA ABIRIA**

MKAZI wa Chang'ombe jijini Dodoma, Juma Hamis (25)...


## Muhimbili yajitosa kutibu ugonjwa unaoathiri ndoa

UKURASA 4

## Hoja ya Gambo yapata watetezi

UKURASA 2


MICHEZO NI YANGA SC VS MWADUI LEO UK.24

MAONI, KATUNI UK.6




Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde (kushoto), akimsikiliza Mbunge wa Jimbo la Segerea, Bonnah Kamoli (katikati), kuhusu maombi ya kujengewa barabara kwa kiwango cha lami, alipofanya ziara katika Kata ya Kisukuru, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Diwani wa kata hiyo, Lucy Lugome. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

## RIPOTI MPYA

# Mapenzi chanzo ajali barabarani

## •Madereva wasafiri na wapenzi

**Na Christina Mwakangale**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limebaini mapenzi ni miongoni mwa sababu kuu za ajali za barabarani zinazohusisha malori nchini.

Mbali na mapenzi, jeshi hilo limevitaja vyanzo vingine vilivyo nyuma ya ajali hizo ni pamoja na uchovu wa madereva, matumizi ya vilevi na kutotumika kwa alama za tahadhari, hasa triangle, kuashiria kuna dharura.

Vilevile, limebaini ajali nyingi hutokea majira ya alfajiri, huku nusu yake zikisababisha vifo na majeruhi.

Takwimu za jeshi hilo zinabainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia miezi minne ya mwanzo (Januari hadi Aprili) ya miaka mitatu (2019 hadi 2021), kati ya malori ya mizigo 843 yaliyopita Barabara ya Morogoro, 546 yalipata ajali na kusababisha vifo 466 na majeruhi 489.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbroad Mutafungwa, anabainisha hayo katika mahojiano na Nipashe jijini Dar es Salaam.

Anataja hatua kadhaa ambazo zinaendelea kuchukuliwa na kikosi hicho kukabiliana na ajali hizo zikijumuisha kutoa elimu kwa madereva na wadau wengine wa barabara wakiwamo wananchi.

Kamanda Mutafungwa anasema wamebaini licha ya kuwapo sheria inayokataza kupakia abiria katika magari hayo, baadhi ya madereva wamekuwa wakiwapakia marafiki zao wa kike, hivyo inapotokea ajali huwa ni sehemu ya waathirika wa ajali.

"Baadhi ya madereva, si wote, ajali hizi kuna uhusiano mkubwa na tabia ya ulevi, madereva wengi nyakati za usiku akisimama sehemu kupumzika, anaingia kwenye starehe baa, anarudi kwenye usukani. Tumewaelimisha kuachana na ulevi," anasema.

Kamanda Mutafungwa anasema ajali hizo kwa kiwango kikubwa hutokea usiku wa manane au alfajiri kwa kutokana na uchovu wa madereva unaochagizwa na wamiliki wa malori kutoajiri madereva wawili wa kupokezana.

Alisema kitaalamu, kila baada ya saa nane, dereva anapaswa kupokewa na dereva mwingine.

"Alfajiri kunapopambazuka kawaida mtu akipigwa na kiubaridi, anasinzia. Dereva huyu aliyechoka atalala muda huu.

"Nyakati za usiku bado tunatoa wito kwamba madereva wote nchini magari yao wanayawekea viakisi mwanga, mkanda kuzunguka gari, pande zote nne, ili kurahisisha kuonekana linapokuwa barabarani hususani usiku.

"Pia kuwapo triangle ili gari likiwa bovu barabarani hasa usiku au dereva mwingine alione.

"Yale ambayo yameharibika pamoja na kuwa na viakisi mwanga, lazima yawe na triangle itakayotumika iwapo gari limeharibika, itawekwa mbele na nyuma, ili dereva mwingine ajue.

"Hivi sasa madereva walio wengi lori likiharibika anaweka majani ambayo hayaonekani.

"Haya magari wakati mwingine huwa yanabeba abiria kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Pamoja na kuwapo kwa utingo ndani ya gari, bado wanapakia abiria kinyume cha taratibu. Abiria aliyepakiwa na utingo ndiyo waathiriwa wakuu wa ajali," anafafanua.

Kamanda Mutafungwa anasema eneo lingine analolitaja kuwapa ugumu katika kukabiliana nalo barabarani, ni madereva wa bodaboda ambao walio wengi baada ya kufanya makosa, hukimbia.

"Tuna operesheni mbalimbali kukabiliana na hali hiyo. Ingawa baadhi ya operesheni nyingine iwapo mtalazimika kumkamata kwa nguvu bodaboda aliyefanya kosa, itamwathiri abiria aliyembeba.

"Tunazingatia ukamataji salama ili isilete athari. Hakuna ukamataji mgumu katika kumkamata bodaboda," anasema.

Kwa kutokuwa na kiakisi mwanga, Kamanda Mutafungwa alnasema adhabu ya dereva ni faini ya Sh. 150,000 au kifungo cha mwaka mmoja gerezani au vyote kwa pamoja.

Anasema magari yote yenye uzito wa kuanzia tani 3.5 lazima yawekwe viakisi mwanga kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani.

**TAKWIMU ZA AJALI ZA MALORI**

| Mwaka | Ajali | Vifo | Majeruhi |
|---|---|---|---|
| 2019 | 331 | 272 | 271 |
| 2020 | 159 | 147 | 152 |
| 2021 | 56 | 47 | 66 |

Hali ya ajali za barabarani zilizohusisha malori katika kipindi cha miezi minne ya mwanzo (Januari hadi Aprili) kwa miaka mitatu mfululizo nchini. **CHANZO: Kikosi cha Usalama Barabarani.**

# Hoja ya Gambo yapata watetezi

**Na Enock Charles**

WADAU wameishauri serikali kurejesha maduka ya kubadilisha fedha (bureau de change) nchini ili kurahisisha huduma kwa wananchi wanaotaka kubadilisha fedha.

Kutokana na hatua zilizochukuliwa na serikali kufunga biashara hiyo hivi karibuni, wadau hao wamesema kwa sasa huduma hiyo imekuwa ngumu kuipata.

Mwanzoni mwa wiki hii, Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo (CCM), aliitaka serikali kurejesha fedha alizodai ilizipoka kwa wafanyabiashara wa maduka ya kubadili fedha mkoani Arusha.

Akizungumza katika mkutano ulioandaliwa na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) jijini Dar es Salaam jana, mwanachama wake, Jabir Idrissa alisema huduma hiyo ya kubadilisha fedha inapaswa kurejeshwa ili kuchochea uchumi na kurahisisha shughuli za wananchi.

"Siku moja nikiwa Zanzibar, nilishuhudia kwenye tawi la CRDB vijana wa kigeni wanafika 20 hivi, wamepanga foleni wanasubiri kubadilisha fedha.

"Ile ni benki ambayo inafunguliwa saa tatu asubuhi, mimi nimeingia kwenye eneo lile saa mbili kama na robo. Kwa hiyo, walikuwa na saa nzima ya kusubiri huduma na hawa ni vijana.

"Pengine walijitolea kuwasaidia watalii wamelala na fedha zao wanataka wabadilishe asubuhi," alisema.

Idrissa alisema kitendo cha huduma hiyo kubakizwa katika benki pekee kimekuwa kikwazo kwa baadhi ya watu wenye shughuli zenye kuhitaji uharaka na pia serikali kupoteza mapato yanayotokana na huduma hiyo muhimu.

Akijibu hoja hiyo, mtaalamu wa fedha wa Taasisi ya Lase Financial Service Limited, Lawrence Mlaki, alisema: "Bado ninadhani bureau de change zipo, baadhi nimeziona bado zipo na benki pia wanafanya hiyo biashara.

"Benki Kuu walishatoa vigezo vya jinsi ya kuomba utaonyesha mtaji na ukikidhi vigezo unaweza ukaomba. Kwa hiyo, ninadhani toka miaka ya nyuma tuliishia hapo, hakuna kingine ambacho tulikisikia kutoka hapo," alisema.

Hoja nyingine iliyoibuka katika mkutano wa TEF jana ni pendekezo la serikali kushusha faini za pikipiki kutoka Sh. 30,000 hadi 10,000.

Baadhi ya washiriki wa mkutano huo walipinga uamuzi huo wa serikali wakidai kuwa asilimia kubwa ya waendesha bodaboda ni wasumbufu barabarani na ni wepesi kuvunja sheria za barabarani, hivyo faini zilipaswa kuongezwa badala ya kushushwa.

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Tawi la Dar es Salaam, Profesa wa Uchumi, Honest Ngowi, aliwasilisha hoja kwa njia ya mtandao kwenye mkutano huo, akitaka suala la ulipaji wa kodi ya majengo kupitia Luku litazamwe kwa kina.

Profesa Ngowi alisema upo uwezekano wa baadhi ya nyumba kulipa zaidi kutokana na kuwa na Luku zaidi ya moja.

Pia, alisema kuna uwezekano nyumba zisizo na umeme na zisizotumia umeme wa Shirika la Umeme (TANESCO) kutojumuishwa katika ulipaji wa kodi hiyo.

Mtaalamu wa Masuala ya Fedha wa Taasisi ya Let's Talk Finance, Edmund Munyangi, alisema hoja hiyo ya Profesa Ngowi ni muhimu kutazamwa kwa kuwa zipo baadhi ya nyumba ambazo zitalipa kodi ya majengo kwa kiwango kikubwa kuliko zingine.

# Mkumbo aanika mkakati wa kurasimisha biashara

**Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Mkumbo (pichani), amesema upo mkakati wa kurasimisha biashara nyingi nchini ili kuongeza fursa ya vijana wengi zaidi kushiriki kujenga uchumi wa taifa.

Aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam alipozindua kitabu cha 'Usimamizi wa Biashara na Fedha' kilichoandikwa na Dk. Fred Msemwa, mjasiriamali na Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Company (WHC).

Waziri Mkumbo alisema takwimu zinaonyesha Tanzania ina zaidi ya biashara ndogo milioni 3.7, lakini ni asilimia nne pekee zilizosajiliwa.

"Tatizo ni ukosefu wa elimu. Kitabu hiki kimeandikwa kwa lugha rahisi, tena kwa Kiswahili. Kitawasaidia wajasiriamali kurasimisha biashara zao.

"Serikali inao mkakati wa kuhamasisha na kufanikisha hilo ili mchango wa kundi hilo uonekane kwenye uchumi wa nchi," alisema.

Kabla ya kumkaribisha mgeni rasmi, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema iwapo wajasiriamali watakuwa na maarifa yanayohitajika kwenye miradi wanayotaka kuitekeleza, benki zitawaamini na kuwawezesha.

"Siku za karibuni, utaanza kuona benki zikikopesha startups (biashara zinazoanza). Kama siyo benki zote, basi CRDB itaifanya hivyo," alisema Nsekela.

Mkurugenzi huyo alisema benki inaweza kumkopesha hata mtu asiye na dhamana lakini mwenye nia ya dhati ya kufanya anachokitamani ingawa sokoni kuna wajanjawajanja wengi.

Akieleza kuhusu kitabu hicho, Dk Msemwa alisema kimebeba uzoefu wake katika ujasiriamali aliouanza tangu akiwa shule ya msingi pamoja na elimu aliyosoma vyuo mbalimbali bila kusahau uzoefu wake kazini.

"Nilianza kufanya biashara tangu nikiwa shule ya msingi. Nilikuwa ninauza mayai ya kuchemsha, miwa na nikapiga picha kijijini pia.

"Nilipomaliza darasa la saba, nilikuwa na akiba ya Sh. 50,000 iliyokuwa inatosha kununua baiskeli mpya 60," alisema.

Dk. Msemwa aliwaeleza waliohudhuria uzinduzi huo kuwa ujasiriamali ni tabia ambayo kila mmoja anaweza kujifunza, hivyo kusimamia biashara yake kwa namna nzuri na endelevu.



# Waziri aagiza mambo sita bandari kuongeza ufanisi

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara (pichani), ametoa maagizo sita kwa uongozi na wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari (TPA) ili kuongeza ufanisi.

Maagizo yake hayo yamelenga kupunguza mianya ya ukwepaji kodi na kuhamasisha uwajibikaji kwa wafanyakazi wa bandari.

Waitara alitoa maagizo hayo jana jijini Dar es Salaam alipozuru kwenye Bandari ya Dar es Salaam na kuzungumza na uongozi na wafanyakazi wa mamlaka hiyo.

Ilikuwa mara ya kwanza kwa kiongozi huyo kukutana na wafanyakazi hao tangu ateuliwe kuwa Naibu Waziri katika wizara hiyo.

Alisema kufanya kazi vizuri kwa watumishi wa bandari kunaisaidia serikali katika ukusanyaji kodi na kuzuia mianya ya upigaji pesa.

"Ninaomba niagize kwamba sisi viongozi wa juu hatutomvumilia mtumishi yeyote yule atakayefanya kazi kinyume cha utaratibu.



"Uzembe, kuwadharau watumishi wapya na kutokuwapa kipaumbele kazini hapa. Ngoja nikazie kidogo, tukileta watumishi wapya hapa wale wazoefu mnawaita hawa watumishi wapya 'wa kuja'. Suala hilo ni marufuku, watumishi wote hapa ni sawa.

"Kufanya kazi bila kuzingatia maslahi ya wananchi, kutotoa taarifa haraka kwa viongozi wa juu pale mnapoona kuna kukwama katika utendaji ndani ya bandari, haikubaliki," alionya.

Waitara pia alionya alichokiita tabia ya baadhi ya wafanyakazi waliopo ndani ya bandari kufanya kazi kwa kusikiliza watu waliopo nje ya bandari.

Pia, alikemea tabia ya baadhi ya viongozi waliopo katika nafasi za juu kupuuza maoni ya wafanyakazi wa chini pamoja na kutokuwapa nafasi za kuwasilisha hoja zao.

"Kumekuwa na baadhi ya viongozi hawana ushirikiano na wafanyakazi wa chini, hii siyo sawa. Ukipigiwa simu pokea, ukitumiwa meseji soma na ujibu.

"Kuna ambayo huwa yanajificha chini kwa chini. Kama ukiwadharau hawa waliopo chini yako, huwezi kupenyezewa habari za upotevu wa mali za umma hapa bandarini.

"Kwa hiyo, ninachopenda nikuone viongozi wakubwa na wadogo mnafanya kazi kwa kushirikiana," aliagiza.

Naibu waziri huyo alifuatana na maofisa mbalimbali wa wizara na mamlaka kukagua na kujionea utendaji unavyoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam.



MAKALA MAALUM

## KUPINDA MGONGO

# Ugonjwa hatari wenye athari lukuki

## •Mabingwa MOI wafichua unavyoathiri uhusiano
## •Waanika hali ilivyo nchini na matibabu yake

**Na Mary Geofrey**

KIBIONGO, kitabibu maarufu scoliosis, ni ugonjwa usiofahamika kama ni tatizo kutokana na jamii kuchukulia kuwa ni hali ya kawaida.

Ni ugonjwa wa kupinda kwa mgongo kunakosababisha kukandamizwa kwa baadhi ya viungo ndani ya mwili wa binadamu hasa mapafu na moyo.

Kupinda huko kwa mgongo kunaelezwa kuwa chanjo cha kutopumua vizuri kwa sababu ya kule kukandamizwa kwa mapafu kutokana na sehemu kubwa ya mgongo inayopinda kuwa nyuma ya kifua.

Nipashe imezungumza na Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Mgongo na Mishipa ya Fahamu katika Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Muhimbili (MOI), Juma Magogo, anayedadavua kwa kina tatizo hili.

Daktari Magogo anasema watu wenye tatizo hilo wanapata pia maumivu makali na haiwaletei picha nzuri katika jamii kutokana na kule kupinda kwao.

Anasema watu wenye tatizo hilo huwafanya kujiona tofauti kidogo na jamii inayowazunguka.

Anasema kuna makundi matatu ya wagonjwa wenye tatizo la kibiongo ambao ni wanaozaliwa na tatizo, wanaolipata kipindi cha ukuaji (rika balehe) na wanaolipata kutokana na kuugua magonjwa mengine yanayohusisha misuli.

Anafafanua zaidi kuwa kwa kundi la wanaozaliwa na tatizo, wakati wa uumbaji tumboni mwa mama, inaweza kutokea baadhi ya pingili za mgongo kushindwa kukaa sawa na zingine au kushindwa kukaa katika ule mgawanyiko unaotakiwa.

Anasema kundi la rika balehe, baadhi mgongo huanza kupinda huku viungo vingine vikiwa sawa. Ingawa hadi sasa watalaamu hawafahamu sababu inayochangia hali hiyo. Anabainisha kuwa kundi la tatu la wanaopata tatizo kutokana na magonjwa mengine waliyowahi kupata yanayohusisha matatizo ya misuli.

### HALI ILIVYO NCHINI

Dk. Magogo anasema hadi sasa Tanzania hakuna takwimu za kitaifa zinazoonyesha hali halisi juu ya tatizo hilo wala idadi ya wagojwa wanaotibiwa.

"Hivi sasa ninakusanya data kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina kuona ugonjwa huu upo kwa ukubwa gani nchini ili pia kusaidia upangaji wa matibabu kwa wagonjwa hawa," anasema Dk. Magogo.

Anasema takwimu za MOI zinaonyesha kwa mwezi huwa wanapokea na kutibu wagonjwa wanne hadi watano, sawa na wagonjwa 48 hadi 60 kwa mwaka.

"Lakini kwa uhalisia tulipaswa kuwa na takribani wagonjwa 200,000 kwa mwaka wanaotibiwa tatizo hili, ambao bado hatujawafikia," anasema.



Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Mgongo na Mishipa ya Fahamu wa MOI, Juma Magogo,

Mtaalamu huyo anasema makadirio hayo wanayapata kwa kulinganisha na takwimu za nchi zingine, akiitolea mfano Marekani yenye idadi ya watu milioni 300 sawa na mara tano ya idadi ya Watanzania.

"Kwao asilimia 1.3 ya idadi yao ya watu ni sawa na wagonjwa milioni nne, ambao wanatibiwa kwa mwaka na asilimia 25 kati yao hutibiwa kwa njia ya upasuaji," anasema Dk. Magogo.

Anasema wakilinganisha takwimu hizo maana yake ni kwamba asilimia 1.3 ya idadi ya Watanzania milioni 60 kulingana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), ni sawa na wagonjwa 800,000 wanaougua ugonjwa huo.

"Tukichukua ile asilimia 25 maana yake ni wagonjwa 200,000 ambao wanahitaji upasuaji kila mwaka nchini, huku tunaita ni 'kuextrapolate', yaani kuchukua data ya nchi nyingine na kulinganisha na nchini mwetu," anafafanua.

Anasema kwa mujibu wa takwimu za idadi ya watu nchini, MOI walipaswa kutibu wagonjwa 200,000 na siyo wagonjwa 40 kwa mwaka.

### WANAWAKE ZAIDI

Dk. Magogo anasema tatizo hilo huwakumba wanawake mara tano zaidi ya wanaume duniani wakati utafiti ukiendelea kufanyika kujua sababu.

Anasema idadi ya wagonjwa MOI wanaume wanahesabika kuanzia watatu hadi watano kati ya wagonjwa wote anaowapokea kwa mwaka.

Anasema utafiti unaendelea japokuwa kuna hisia kwamba pengine linahusiana na masuala ya homoni au vinasaba kwa wanawake japo kuna magonjwa mengine unakuta wanaume ni wengi zaidi kuliko wanawake.

Anafafanua zaidi kuwa mara nyingi kinamama ndiyo huwa wa kwanza kuwagundua watoto wao, kipindi wanapowaogesha, kuwanunulia nguo mpya au viatu, huhisi na kuona mabadiliko katika migongo (miili) ya watoto wao.

"Kama ameota matiti, moja linakuwa limesogea mbele kuliko lingine, au anakuwa bega moja limepanda juu kuliko lingine au anaona kupinda kwa mgongo," anasema Dk. Magogo.

Anaeleza kuwa mtoto anapokuwa ameketi na wenzake yeye hujipinda zaidi, mtoto huwa mchaguzi wa viatu, hukataa kuvaa viatu virefu kwa sababu anapovaa huhisi maumivu makali ya mgongo, hivyo hupendelea kununuliwa na kuvaa viatu vya chini.

### TIBA MAZOEZI

Daktari Bingwa huyo anasema pamoja na tiba ya upasuaji, tatizo hilo linaweza pia kutibika kwa njia ya tiba mazoezi, ikiwa litagundulika katika hatua za awali.

Anasema tatizo hilo linatibika na kupona vizuri zaidi mtoto akiwa katika umri huo wa miaka tisa hadi 14.

Anasema wanatumia vipimo vya CT-Scan na X-ray kuangalia limefikia hatua gani kwa kuwa vipimo hivyo huwezesha kuangalia mgongo kuanzia hatua ya shingo hadi kwenye mkia.

Daktari huyo anasema kwa vipimo hivyo wanaweza kujua 'angle' ambayo huwasaidia kuchagua aina ya matibabu kwa mgonjwa.

"'Angle' ya kupinda ikiwa chini ya 25 mgonjwa anaweza kutibiwa kwa njia ya tiba mazoezi.

"Tunaweza kumpa muda na kumfuatilia kwa kipimo maalum ambacho kinaweza kutumika hata nyumbani na shuleni, anakuwa anashika magoti na kuinama, tunamwelekeza mama, mwalimu jinsi ya kumpima 'angle'. Ikiwa itaonekana linaongezeka, anamrudisha hospitali," anasema Dk. Magogo.

Anaeleza kuwa inapobainika ana tatizo, ikiwa kuanzia 60 na kuendelea hapo haiwezekani tena kutibu kwa mazoezi, bali huhitaji upasuaji ili kuzuia kuendelea kupinda kwa mgongo wake.

"Kwa sababu asipofanya upasuaji anaendelea kuwa na maumivu, anaathirika kisaikolojia, anazidi kunyanyapaliwa, anashindwa kujiamini kuingia kwenye uhusiano, hususani wasichana wanaathiriwa mno kisaikolojia na tatizo hili," anafafanua Dk. Magogo.

Anasema kisayansi mgongo utaendelea kupinda, moyo na mapafu yatazidi kukandamizwa na ikiwa mapafu ndiyo yaliyokandamizwa atazidi kupata shida ya upumuaji, ataishi na maumivu makali na ikiwa moyo utakandamizwa kuna uwezekano mkubwa kwa mgonjwa kupoteza maisha.



# TPB yazindua bima maisha kwa wateja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya TPB kwa kushirikiana na Kampuni ya Bima ya Alliance Life Assurance, imezindua bima ya maisha kwa wateja wenye akaunti binafsi katika benki hiyo ambalo ni fao linalotolewa kwa wateja wao.

Katika bima hiyo matukio yaliyohusishwa ni kifo cha mteja, mwenza wake na ulemavu wa kudumu kwa mteja unaotokana na ajali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Kitengo cha Bima wa benki hiyo, Francis Kaaya, alisema kuna mafao mawili ambayo yatakuwa yanatolewa ikiwamo fao la kifo na ulemavu wa kudumu.

"Fao la kifo ni kwa mteja mwenye akaunti ya akiba dhidi ya tukio la kifo cha mmiliki wa akaunti, mwenza na watoto wasiozidi wanne, Benki ya TPB itatoa kifuta machozi kwa wateja au familia kama rambirambi ili kutatua baadhi ya gharama zinazohusiana na mazishi.

"Kwa upande wa fao la walemavu wa kudumu, hili linapatikana kwa mteja ambaye ni mmiliki wa akaunti anayekabiliwa na ulemavu wa kudumu uliotokana na ajali, benki itatoa mkono wa pole kumsaidia mwathirika aliyekumbwa na tatizo au familia yake ,"alisema Kaaya.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa TPB, Sabasaba Moshingi, alipongeza uongozi wa Alliance Life Assurance kwa kugundua umuhimu wa huduma hiyo kwa wateja wao.

"Benki ya TPB inatambua umuhimu wa bima katika maisha ya kila binadamu na kwa sasa nchi yetu inakabiliwa na ufinyu wa watu kujiandikisha na bima mbalimbali, huduma hizi hazitakuwa na gharama ya juu kwa mfano kwa fao la kifo mteja atapata Sh.milioni mbili, mwenza wa mteja pia atapata kiasi hicho na watoto wa mteja wasiozidi wanne kila mmoja ni milioni moja na kwa upande wa fao la ulemavu wa kudumu ni mteja tu atapata milioni mbili ,"alifafanua Moshingi.

Alisema mambo ya kuzingatia ni pamoja na mnufaika kuwa mteja wa Benki ya TPB mwenye akaunti ya akiba.

"Akaunti lazima iwe hai, hakuna kipindi cha kusubiri, hakuna kikomo cha umri, vifo vya asili na vya ajali vinalipiwa na mdai lazima awasilishe maidai yote," alisema.

# Kondakta auawa kwa jiwe wakigombea abiria

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKAZI wa Chang'ombe jijini Dodoma, Juma Hamis (25) ambaye ni kondakta wa daladala amefariki dunia baada ya kudaiwa kupigwa jiwe kichwani na dereva wa daladala wakati wakigombea abiria.

Tukio hilo lilitokea juzi katika Kituo cha Daladala cha Chang'ombe jijini hapa, ambapo dereva huyo alikuwa anaendesha gari lingine linalofanya safari zake za Chang'ombe kwenda mjini akidaiwa kumpiga jiwe kisogoni.

Mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, Ally Said, alidai kuwa dereva huyo aliyetajwa kwa jina moja la Hussein, alimpiga jiwe kisogoni kondakta huyo wakati akifungua mlango wa daladala.

Alidai ilikuwa kawaida kwa kondakta huyo kutaniana na makondakta wenzake wakiwa kituoni kuita abiria.

Hata hivyo, siku ya tukio, dereva alimfuata huku akiwa kashika jiwe na kumpiga nalo kisogoni akiwa amesimama kwenye mlango wa daladala.

Said alidai kuwa baada kupigwa jiwe, kondakta huyo alianguka chini ndipo wasamaria wema kituoni huko wakiwamo makondakta wenzake, walimchukua na kumkimbiza kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Alidai kuwa baada ya kumfikisha katika hospitali hiyo, muda mfupi baadaye waliambiwa kuwa kondakta huyo alikuwa ameshafariki dunia.

Akizungumza kwa niaba ya familia, mjomba wa marehemu, Ramadhan Said, alisema wamepokea kwa masikitiko kifo cha ndugu yao kwa sababu hakuwa na tabia za ugomvi bali utani.

Alidai dereva aliyefanya kitendo hicho alikimbia baada ya tukio.

Hata hivyo, alisema wanamwomba Mungu awape subira wakati wakisubiri Jeshi la Polisi likiendelea na msako kumpata aliyefanya kitendo hicho cha kikatili dhidi ya ndugu yao.

"Hapa mtaa wa jirani amekimbia katika nyumba anayoishi na haijulikani amekwenda wapi, tunasubiri mkono wa sheria ufanye kazi yake juu ya tukio hilo," alisema.

Alibainisha kuwa mwili wa Juma (25) ulizikwa katika makaburi ya Nkuhungu jijini Dodoma na ameacha mke aliyefunga naye ndoa miezi mitatu iliyopita.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo, akisema Jeshi la Polisi linaendelea na msako kumtafuta mtuhumiwa aliyetenda kosa hilo.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo ya mradi wa ujenzi wa Kituo cha Polisi Chang'ombe, kutoka kwa Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Zakaria Senso, baada ya kuweka jiwe la msingi, jijini Dodoma jana. Wa pili kulia ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Ramadhani Kailima. **PICHA: WMNN**

# Kamera kukabili uhalifu Dodoma

**Na Romana Mallya, DODOMA**

UONGOZI wa Mkoa wa Dodoma umesema kamera za usalama zitafungwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma ili kupunguza uhalifu ambao umeanza kushamiri.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alibainisha kuwapo kwa mkakati huo jana wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Kituo cha Polisi Chang'ombe jijini humo.

Ujenzi wa kituo unatekelezwa kutokana na kukithiri kwa vitendo vya uhalifu ikiwamo uporaji, ubakaji, udhalilishaji na matumizi ya dawa za kulevya katika maeneo ya Chang'ombe na kusababisha wananchi wa maeneo hayo kuishi kwa wasiwasi.

Mtaka alisema watafunga kamera maeneo mengi ya jiji hilo.

"Hatuwezi kuwa na jiji ambalo polisi wetu wanakimbizana na wahalifu muda wote, tutatumia teknolojia hiyo kudhibiti uhalifu wa aina mbalimbali.

"Dodoma ni Makao Makuu ya nchi, lazima pawe salama, ninawashauri wahalifu watafute shughuli nyingine ya kufanya, hapa si salama tena kwa kazi zao," alisema.

Kuhusu kituo hicho cha polisi, Mtaka aliwataka wananchi kushirikiana na serikali kuhakikisha ujenzi wake unakamilika mapema ili kianze kutoa huduma za kiusalama katika maeneo hayo.

"Chang'ombe inakua, inahitaji kituo kikubwa kitakachofanya kazi saa 24 ili wafanyabiashara na wananchi wafanye shughuli zao kwa muda wote na siyo biashara zifungwe kwa kuhofia uhalifu.

"Sasa kazi ya serikali siyo kukwambia ufunge biashara yako muda gani, kazi ya serikali ni kukulinda ili kuwapo uhuru wa kutoa huduma. Kwa hiyo, wananchi tushirikiane ili kituo kimalizike haraka," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Katibu Mkuu, Ramadhani Kailima, alisema wizara imetoa Sh. milioni 10 kama mchango wake katika ujenzi wa kituo hicho na kikikamilika kitatoa huduma mbalimbali ikiwamo upelelezi wa matukio, upelekaji wa majalada ya kesi kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka ili watakaothibitika na makosa wafikishwe mahakamani.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde (CCM), alichangia papo hapo mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi huo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Uamuzi fedha za TPA, TCRA na TASAC kuwekwa akaunti maalum uungwe mkono

**SERIKALI** katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2021/22 inayotarajiwa kupitishwa keshokutwa, pamoja na mambo mengine, imeomba kuweka kwenye akaunti maalum katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT) mapato ya baadhi ya taasisi za umma zikiwamo Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA) na Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC).

Kuanzishwa kwa akaunti hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika kudhibiti matumizi kwenye mashirika na taasisi za umma. CAG katika ripoti yake ya mwaka 2019/20, anapendekeza serikali kuzibana taasisi zake katika kudhibiti matumizi ya fedha ili kukuza uwazi, uwajibikaji na utawala bora.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Wajibu na CAG mstaafu, Ludovick Utouh, alibainisha wiki hii katika taarifa ya uchambuzi wa bajeti hiyo kwamba mpango huo umezingatiwa kutokana na mapendekezo hayo ya CAG.

Hatua ya mapendekezo hayo ilitokana na kubainika kwamba kumekuwapo na matumizi mabaya ya fedha za TPA huku takriban Sh. bilioni mbili zikitumika kugharamia vikao vya bodi za baadhi ya taasisi.

Hatua hiyo, alisema inaonyesha serikali imezingatia mapendekezo ya CAG katika ripoti yake iliyowasilishwa bungeni Aprili, mwaka huu. Kutokana na mapendekezo hayo, mapato ya TPA, TCRA na TASAC kuanzia mwaka ujao wa fedha yatakuwa yakikusanywa na taasisi hizo kupitia mfumo wa GePG na kuingizwa kwenye akaunti za makusanyo zilizoko BoT. Ripoti ya CAG iliyowasilishwa bungeni Aprili, mwaka huu, ilibainisha upotevu wa Sh. bilioni 3.93 kutokana na miamala ya udanganyifu katika bandari za Kigoma na Mwanza kutokana na udhaifu wa mifumo ya ndani katika usimamizi wa malipo. Sambamba na hiyo, ripoti ilibaini TASAC kufanya vikao 20 vya bodi ya wakurugenzi katika mwaka mmoja wa fedha jambo ambalo ni ukiukwaji wa kanuni za uendeshaji wa mashirika na taasisi za umma.

Kwa kawaida, vikao vya bodi vinatakiwa kufanyika mara moja kila robo mwaka, sawa na vikao vinne kwa mwaka. Kufanyika kwa vikao hivyo, kulisababisha matumizi ya takriban Sh. bilioni mbili.

Uamuzi wa serikali kuazimia mapato ya taasisi hizo kuwa na akaunti maalum BoT ni wa kuungwa mkono kwa kuwa utasaidia kuongeza mapato ya serikali na wakati huo huo, kudhibiti mianya ya ubadhirifu na matumizi mabaya ya fedha. Licha ya kudhibiti, pia ni hatua nzuri ya kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika mashirika ya umma.


Huo ni mwanzo mzuri lakini ni vyema wigo zaidi ukapanuliwa katika udhibiti ili kuhakikisha fedha zaidi zinakusanywa na kuelekezwa katika miradi mbalimbali na kwa maendeleo ya taifa kwa ujumla.

Kabla ya kuingia kwa uchumi wa soko, kulikuwa na Kamati ya Usimamizi wa Mashirika ya Umma (SCOPO) ambayo pamoja na mambo mengine, ilikuwa na jukumu la kupanga mishahara ya mashirika pamoja na usimamizi wa fedha.

Hatua hiyo ilisababisha kuwapo kwa nidhamu katika uendeshaji mashirika na waliokuwa wakibainika kuvurunda walikuwa wakichukuliwa hatua. Lakini baada ya hapo usimamizi wa mashirika ya umma ulikuwa chini ya Msajili wa Hazina ambaye kwa kiasi kikubwa ameonekana kushindwa kutekeleza jukumu hilo.

Kwa ujumla, tunaunga mkono uamuzi huo na Bunge katika kuhitimisha mjadala wa bajeti liunge mkono jambo hilo kwa kuwa lina manufaa kwa taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ushiriki huu wa wananchi wafaa kuigwa



Na Sabato Kasika

**MOJA** ya miradi ambayo imekuwa ikitekelezwa na serikali, ni pamoja na kuendelea kujenga zahanati kila kijiji, kituo cha afya kwa kila kata, ili kusogeza huduma ya afya karibu na wananchi.

Katika mradi huo wa ujenzi wa zahanati kila kijiji, wananchi na kwenye baadhi maeneo, wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi hizo za serikali kwa kutoa ngvukazi zao au fedha ili kufanikisha ujenzi huo.

Hatua hiyo inatokana na ukweli kwamba, sekta ya afya ni moja ya sekta nyeti kwa mustakabali wa maisha ya jamii, kwa kuwa mtu anapokuwa afya bora inaweza kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kujiletea maendeleo.

Umuhimu huo wa afya ndiyo unaowafanya baadhi ya watu kuwa mstari wa mbele kushirikiana na serikali katika kufanikisha ujenzi wa zahanati katika vijiji vyao na hata vituo vya afya kwenye kata zao.

Shughuli za ujenzi wa zahanati na vituo vya afya zinaendelea katika maeneo mbalimbali nchini huku wananchi wakijitolea kusomba maji, mawe, kokoto na mchanga na wakati mwingine kuchangia fedha taslim.

Wananchi wanaofanya hivyo, ni wale ambao wanaelewa umuhimu wa wao kushiriki katika kuboresha huduma za afya kwenye maeneo yao badala kusubiri kufanyiwa kila kitu.

Miongoni mwa maeneo ambayo wananchi wamehasishwa na kuunga mkono juhudi hizo za serikali, ni Wilaya ya Musoma mkoani Mara, ambako wameshiriki katika ujenzi wa zaidi ya zahanati 20.

Mbali na hizo, zingine 15 zinaendelea kujengwa katika vijiji mbalimbali kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zanahati ili kutimiza lengo la serikali la kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Vimcent Anney, anasema ni hatua ya kujivunia kwa kuwa wananchi wanatambua umuhimu wa kushiriki katika shughuli za maendeleo kwa ajili yao.

Kimsingi afya ni rasilimali muhimu kwa binadamu, hivyo hatua ambazo zinachukuliwa na wananchi wa maeneo hayo kwa kutoa nguvukazi yao na fedha ili kujenga zahanati na vituo vya afya ni za kuigwa.

Kwa kuwa serikali imekuwa ikitoa fedha katika halmashauri nchini, kwa ajili ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya na hospitali za wilaya, ushiriki wa wananchi katika ujenzi huo ni wa muhimu.

Ushiriki wao unasaidia kutimiza azma ya serikali ya kusogeza huduma za afya karibu yao ili waondokane na usumbufu wa kusafiri au kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Wakati wananchi wanashirikishwa katika ujenzi huo, ingependeza kama zahanati, vituo cha afya na hospitali, ambavyo zimekamilika vyote vikawa na vifaa tiba, watumishi wa kutoa ili kuwapo kwa huduma zinazotakiwa.

Iwapo dawa, vifaa tiba na madaktari na watumishi wengine hawatakuwepo, hali hiyo inaweza kuwakatisha tamaa wananchi, ambao wamekuwa wakitoa nvuvukazi na fedha zao katika ujenzi huo.

Kwa mfano, Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi ina uhaba wa watumishi wengi wa kada ya afya, hali ambayo inasababisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi kuwa mgumu.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Hassan Rugwa, kabla ya kuteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam hivi karibu, aliwahi kuelezea idadi ya watumishi waliopo. Aliweka bayana kamba wilaya hiyo inahitaji kuwa na watumishi wa kada ya afya 1077, lakini waliopo ni 305 hali inayosababisha baadhi ya zahanati kutokuwa na watumishi au kuwapo wawili au mmoja.

Mazingira ya aina hiyo yanaweza kusababisha wananchi wanaojitolea kujenga zahanati na vituo vya afya kukata tamaa, kwa kunadhini kuwa wanapoteza nguvu zao kwa jambo ambalo halina manufaa kwao.

Wakati wakiendelea kushiriki katika ujenzi huo, wahusika wa ajira kwa upande wao siyo vibaya kuweka mazingira ya kuandaa watumishi wa kutosha watakaopelekwa kwenye zahanati hizo au vituo vya afya.

Wataalam wa afya wanasema kuwa kwa kawaida zahanati inatakiwa kuwa na watumishi kuanzia nane hadi 10, na kituo cha afya kinatakiwa kuwa na watumishi kuanzia 28 hadi 30.

Kwa hesabu hiyo ni kwamba, wilaya ya Musoma yenye vijiji 68, inatakiwa kuwa na watumishi kati ya 544 hadi 680 iwapo kila kijiji kitakuwa kimekamilisha ujenzi wa zahanati yake.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hongera DPP, kazi imeanza vizuri, iendelee...



Na Pascal Mayalla

**Mahabusu zetu ni mahali hatarishi, na kutokana na umasikini wetu, hatuna magereza ya mahabusu (remand prison) na jela ya wahalifu, mahabusu wetu wanashikiliwa jela kama wafungwa. Wapo ambao wamepata matatizo ya kiafya permanently (kudumu) kwa kurundikana mahabusu bila huduma za msingi ambapo wangeweza kujihudumia wenyewe wawapo nje.**

UNAPOANDIKA makala kulalamikia jambo fulani, na kutoa ushauri wa nini kifanyike, halafu ikatokea hicho ulichoshauri kikafanyika, kama ulivyoshauri, hatua ya kwanza ni kutoa pongezi, kwa hicho kilichofanyika, hivyo makala ya leo, naianza kwa kumpongeza DPP, ametenda! Kumbe Kutenda haki kunawezekana, hongera DPP mpya kwa kuanza vizuri, na sasa kazi hii nzuri, iendelee, na sio kusubiri tena hadi Mama aseme!

Sasa naendelea na ule ushauri wa DPP, wiki iliyopita niliishia number sita, leo naendelea.

Kuna watuhumiwa wako mahabusu kwa makosa yanayodhaminika, bali DPP ameiamuru mahakama kuzuia dhamana zao.

Hapa kuna mambo matatu. Moja ni masuala ya weledi, haki na uwajibikaji wakati wa kutekeleza mamlaka kwa mujibu wa kifungu hiki. Mbili ni uhalali wa kifungu hiki kikatiba ambacho kwa kweli hakitoi uwajibikaji kabisa ndiyo maana kilifutwa kwenye CPA baada ya mahakama kujiridhisha kifungu hiki kinakwenda kinyume cha Katiba, kisheria, mahakama ikiishatoa amri, sheria fulani au kifungu fulani kiko kinyume cha Katiba, na kifungu hicho kifute, kifungu hicho kinakuwa "null and void abinitio", yaani hakukuwahi kuwapo.

Lakini kwenye kufutwa kwa kifungu hiki, kuna kitu cha ajabu kimetokea, wakati kifungu hiki kimefutwa na mahakama kwa kuwa kinyume cha Katiba kwenye CPA, kifungu hicho bado kipo kwenye EOCCA! Hili ni jambo la ajabu sana! Hapa naiomba Mahakama itamke kifungu fulani kinakwenda kinyume cha Katiba, na kuamuru kifutwe, kifungu hicho kifutwe kwenye sheria nyingine zote.

Sasa tunaishi kwenye ulimwengu wa kidigitali, Tanzania na sisi tutumie nafuu za kidigitali, kwa kuanzisha 'digital custody' mahabusu za kidigitali na 'digital cells', jela za kidigitali, mtuhumiwa anazuiliwa nyumbani kwake, hata kutumikia kifungo akiwa nyumbani kwakwe kwa kufungiwa kifaa maalum cha GPS (tracking device), inayofungwa kwa lakiri ya kidigitali, na kuzuiwa nyumbani kwake, nyumba hiyo inafungwa kamera, maalum (IP Camera) kama zile za CCTV, hivyo Polisi/Magereza wanaona nyendo zote za mtuhumiwa, akivuka tu, ile IP camera, inapiga alarm (tahadhari), mtuhumiwa anakuwa amekiuka masharti hivyo kustahili kuzuiliwa mahabusu. Utaratibu huu unaruhusu mke kupata haki zake za ndoa, watoto kupata mapenzi ya baba, na baba kuendelea na shughuli za kuingiza kipato cha kuendesha familia.

Mahabusu ni mtuhumiwa tu, anahesabika hana hatia hadi athibitishwe na mahakama, lakini mahabusu wetu, wanahesabiwa kama wafungwa, wananyimwa haki zao, mfano watuhumiwa wengi tu ambao sio hatarishi wamefiwa na ndugu zao, wazazi wao, wapendwa wao au jamaa zao, bila kupewa haki ya kushiriki mazishi yao, mfano mwanahabari Erick Kabendera, alifiwa na mama yake akiwa mahabusu na hakuruhusiwa kumzika. Sisi watu wa karma, tulitoa angalizo la karma ya huyu mama, wanaojua karma ilikuja kufanya nini, wanajua!

Mahabusu zetu ni mahali hatarishi, na kutokana na umasikini wetu, hatuna magereza ya mahabusu (remand prison) na jela ya wahalifu, mahabusu wetu wanashikiliwa jela kama wafungwa. Wapo ambao wamepata matatizo ya kiafya permanently (kudumu) kwa kurundikana mahabusu bila huduma za msingi ambapo wangeweza kujihudumia wenyewe wawapo nje.

Japo hapa natetea haki za watuhumiwa, pia naomba pia kuzingatia haki za wahanga wa uhalifu. Katika ulimwengu wa uhalifu kuna watu wabaya kupita kipimo.

Just imagine (fikiria) unakuta mtu mzima umembaka mtoto wa miaka miwili na kumharibu na pengine akamwambukiza HIV, mauaji ya kutisha, vitendo vya vikundi vya kihalifu kama panya road na mapanga yao wanapokuingilia na kukucharanga mapanga bila huruma na kumbaka binti yako au mkeo mbele yako na visa vingine vingi.

Hao ni ma 'psychopath' wanastahili kukaa mahabusu kwasababu ni watu hatarishi, wasipate dhamana kwa vile wamepoteza sifa za haki yao kuwa huru.

Ule utaratibu wa notification kwa makosa ya usalama barabarani, na kulipa faini za papo kwa papo, utumike pia kwenye vituo vya polisi, mwizi wa kuku, akubali kumlipa aliyemuibia na kulipa faini, kesi hiyo inaishia hapo hapo kituoni wala haina haja ya kufikishwa mahakamani.

Majaji wetu kwa ajili ya kusikiliza maombi ya dhamana, nao wanapaswa kufanya kazi kama vituo vya polisi, hospitali na dharura nyingine kwa saa 24.

Kama ilivyo kwa madaktari wa zamu anapigiwa simu kukitokea dharura, kuwe na majaji wa zamu saa 24/7. Nimeshuhudia hii Afrika Kusini, kila mtuhumiwa anapelekwa kwa hakimu wakati wowote hadi usiku wa manane, kama vile madaktari au vituo vya polisi.

Mwisho, Mheshimiwa DPP wetu mpya, hongera kwa uteuzi wako mpya, Watanzania tuna matumaini makubwa sana na Rais wetu Mama Samia katika nia yake ya dhati kutaka Watanzania watendewe haki, na amekuaminia wewe kuongoza na ofisi hii muhimu sana, ya DPP, timiza wajibu wako kwa mujibu wa Katiba, sheria, taratibu na kanuni, kama ulivyoanza, Taifa litaponywa kwa haki.

**Mungu Ibariki Tanzania.**
**pascomayalla@gmail.com**
**0754270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Uviko yuko kona anachungulia upenyo



Na Joseph Kulangwa

**Kuna wakati nikiwaangalia Watanzania a.k.a Wabongo, huwa najiuliza mara mbili kama tuko sawa kiakili, au pengine bongo zetu zinahifadhiwa mahali na watu wengine, kwa sababu hatujali mambo yetu. Tunakwenda tu kama nyumbu, ambao akitangulia mmoja, hata upige bomu katikati watafuata njia hiyo tu.**

HAKUNA viumbe wenye michezo mingi kama watoto wadogo. Hawa kwao kila kitu ni kucheza hasa wanapokuwa wameanza kukaa, kusimama dede au kutembea. Zamani tukiwa wadogo, tulicheza michezo ya kujipikilisha, kujificha, kibaba na mama, hata kuchezea wadudu bila kujua wana athari chanya au hasi, mpaka hapo tulipong'atwa, ndipo tuliacha kuwachezea.

Mfano kuna nyakati tulishuhudia sisimizi, mchwa au sungusungu au chungu, wakiwa kwenye msafara wao, nasi kwa makusudi na ukatili mkubwa, tulikanyaga kati ya msafara au kupiga kwa fimbo na msafara ukasambaratika.

Tulifurahi sana kuona sisimizi, mchwa au chungu, wakipoteza mwelekeo, bila kujua tuliwasababishia usumbufu, hasara na misiba, kwani baadhi yao walipoteza maisha kwa mchezo wetu huo. Tulifurahi wao wakiomboleza.

Tulishuhudia lakini pale pale wakijipanga na kuondoa wafu njiani na kuendelea na msafara kana kwamba hakuna kilichotokea. Kwa binadamu likitokea hilo, mathalan ukisoma hadithi za wale watu wa Liliput ambao walikuwa wadogo mithili ya sisimizi, walikanyagwa na mijitu mikubwa na kuangamia.

Binadamu alijiuliza na kukatiza kama si kufuta msafara ule na kushughulikia maziko ya ndugu waliokumbwa na gharika la kukanyagwa na mijitu ile. Sisimizi wala, waliendelea na msafara.

Kuna wakati nikiwaangalia Watanzania a.k.a Wabongo, huwa najiuliza mara mbili kama tuko sawa kiakili, au pengine bongo zetu zinahifadhiwa mahali na watu wengine, kwa sababu hatujali mambo yetu. Tunakwenda tu kama nyumbu, ambao akitangulia mmoja, hata upige bomu katikati watafuata njia hiyo tu.

Nchi hii ilishakumbwa na magonjwa mengi sana, yaani yawezekana kila gonjwa lililoumbwa duniani lilishapita Tanzania na kuondoka na waja wake. Si kipindupindu, malaria, ukoma, ndui, polio, UKIMWI, denge na sasa uviko.

Magonjwa yote haya yakiingia hututikisa kama ambavyo mchwa wanapokuwa amekatizwa msafara wao. Tunahaha huku na kule, na hatimaye tunasahau mara na maisha kuendelea kana kwamba halijatokea jambo. Lakini tunakufa na tunafiwa!

Hapo ndipo ilipo ajabu ya Wabongo hawa. Angalia hivi karibuni tu hapa, Corona ikatuhenyesha, tukalia, tukakataana hata kwenye kuzikana. Kila kona ikawa Corona! Corona! Watu wakaambiwa vaeni barakoa, msichangamane, kaeni mbalimbali, tukafundishwa hata namna ya kupiga chafya na kukohoa, kana kwamba hatukuzaliwa tukijua.

Yote hayo yakifanyika ili kuokoa maisha. Tukisikia kwa wenzetu huko wanafungiana, hakuna kutoka. Hapa tukasema tukifungiana ndipo tutakufa vizuri, tuache tu ila tujihadhari. Tukaenda mbali mpaka baadhi ya wakuu wa mikoa wakakataa Watanzania wenzao. Wakihanikiza hakuna mtu wa mkoa mwingine kuingia mkoa mwingine!

Viongozi wakahaha kutafuta dawa ya kupambana na Mzee Uviko, wakakumbuka tangawizi zinazochanganywa na pilipili kichaa na vitunguu swaumu, ukali wake gongo cha mtoto. Lakini kwa kuogopa kifo watu wakafakamia hivyo hivyo. Wengine wakatumia fursa hii kuonesha kuwa ni wajuzi wa tiba. Taasisi ambazo miaka nenda rudi hatukuwa tumesikia uvumbuzi wao, nazo zikaibuka.

Tukanyweshwa michanganyikio mbalimbali ya mimea, ili mradi Uviko atuache kama alivyotukuta. Baadhi ya wanasiasa wakaanza kutoa kauli za ajabu ajabu, oh Uviko lazima uishi Tanzania kwa nidhamu! Ikawa sasa ni futuhi, nchi nzima futuhi.

Nyungu huku nyungu kule, watu wakajifukiza utadhani ile dawa ya kuua mbu iliyokuwa ikichomwa huko nyuma, tukiambiwa inatokana na mavi ya tembo. Ikiitwa Tembo coil. Nani anakumbuka hiyo? Nyungu ikatolewa kwa awamu, mawaziri nao wakatafutia ujiko huko.

Hatimaye eti tukaambiwa tuombe siku tatu bila kula. Tukafanya hivyo, wakasema Mungu katusikia sasa mambo bulbul. Tukabweteka. Uviko akachungulia akaona upenyo, akarudi akapiga pigo moja nyoofu, kama la Umsolopagaas, baadhi ya viongozi wakapatwa, wengine wakaaga. Msafara umeingiliwa. Tukafunguka macho. Sasa tumeyafumba tena.

Tunadhani mambo bado bulbul, msafara unaendelea. Uviko yuko kwenye kona anatafuta upenyo mwingine, akirudi atachukua baadhi yetu, tukishituka tumechelewa. Tuchukue hadhari jama. Uvikio hajachoka.

**Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Wanasiasa wa aina hii tuwe nao makini kuelekea 2025



Na Thobias Mwanakatwe

**Lakini kwa kizazi hiki cha Kitanzania, ni lazima tuwaambie, kwa nini tunawapa madaraka. Mwanasiasa anapanda jukwaani anawaambia wananchi kuwa, "Tanzania ni nchi mojawapo Kusini mwa Jangwa la Sahara yenye matumizi ya chini sana ya mbolea katika ngazi ya wakulima wadogo.**

MIONGONI mwa mambo yanayonitatiza ni uwasilishaji wa hotuba au michango ya baadhi ya wanasiasa nchini. Imezoeleka kwa wanasiasa kutumia maneno ambayo hayana tija kwa wapigakura wao. Wanapigania maeneo ambayo hayagusi maisha ya wananchi.

Mara nyingi mambo haya yamekuwa yakijitokeza zaidi bungeni ambako imekuwa kawaida mfano mbunge wa upinzani na chama tawala kupigana vijembe.

Utamaduni mpya uliojitokeza na ambao haujazoweleka ni wa baadhi ya wabunge kufikia hatua ya kuwasema vibaya baadhi ya viongozi wakuu wa kitaifa waliotangulia mbele ya haki.

Mambo kama hayo yamekuwa mengi. Staili ya uwasilishaji wa wanasiasa wetu licha ya mipasho au vijembe, bado tunakabiliwa na tatizo kubwa la uwasilishaji wa mawazo mbadala.

Hata tunapowasikiliza kwenye mikutano ya kuomba kura au ya hadhala ya vyama vya siasa ambayo hivi sasa inaendelea ni rahisi kubaini kuwa hawana ajenda au mambo yaliyopaswa kuzungumzwa miaka 20 iliyopita yanaendelezwa leo.

Sasa basi, kwenye suala la mabadiliko ndani ya nchi hii yanapaswa kuanza na wanasiasa wenyewe kwenye mwenendo wao wa kila siku kuendesha siasa kwa ujumla wake au walazimishwe kubadilika.

Katika ulimwengu wetu huu, lazima tufahamu kuwa hata wale ambao wanatusikiliza kwenye mikutano yetu au vikao vya bunge, wanao uwezo wa kuelewa mantiki zinazowasilishwa. Wananchi waliopaswa kuambiwa maneno yasiyofaa ambayo hayana tija na si kipaumbele chao katika jimbo lao hilo ni tatizo.

Lakini kwa kizazi hiki cha Kitanzania, ni lazima tuwaambie, kwa nini tunawapa madaraka. Mwanasiasa anapanda jukwaani anawaambia wananchi kuwa, "Tanzania ni nchi mojawapo Kusini mwa Jangwa la Sahara yenye matumizi ya chini sana ya mbolea katika ngazi ya wakulima wadogo.

Huu ni mfano wa dhahiri ambao mwanasiasa anatakiwa kuzungumzia kokote anendako. Awaambie wananchi (ambao kwa kiasi kikubwa sasa kiwango cha uelewa wa wapigakura kimekua zaidi, hususani wapigakura waliozaliwa miaka 1990 kuelekea karne ya 21).

Wananchi au wapigakura wa namna hii si wa kuwaletea vijembe pekee, bali wanachambua maudhui ya hotuba zenu na kuweka mizani.

Haiwezekani katika karne ya 21 mwanasiasa anatumia dakika nyingi kushusha vijembe na kuondoka kisha akaita huo ni mkutano wa hadhara. Badala yake sitakosea nikisema hakuna tofauti na vijiwe vya kahawa kwenye mikutano mingi ya wanasiasa nchini.

Mwasiasa anakwenda kuzungumza na wananchi wa Rukwa, anatakiwa kujua changamoto zilizoko huko. Anakwenda kuzungumza na wananchi wa Kigoma, anatakiwa kujua hatima ya kilimo na kiwanda cha mawese.

Mwanasiasa akienda Mtwara, anatakiwa kujua kinachoendelea katika suala la korosho. Mwanasiasa akifanya ziara mjini Tukuyu, mkoani Mbeya, anatakiwa kuzungumzia maendeleo ya biashara ya ndizi na parachichi kwa wakulima.

Mwanasiasa wa kizazi kipya anatakiwa kuzungumzia habari za uchumi na maendeleo. Habari za ufanisi wa miradi na utekelezaji wa mikakati. Pia anatakiwa kujua kuwa habari nazo huamua hatima ya upigaji kura. Ongezeko la matumizi ya mitandao ya kijamii limechochea ukubwa wa upatikanaji wa habari.

Maeneo ambayo hayakuwahi kufikiwa na wanasiasa wayazungumze wananchi wenyewe kupitia soko la habari. Wananchi wakija kukusikiliza mwanasiasa hakikisha huleti habari za "tunapigana kila njia kuhakikisha kesi ya mwanasiasa fulani aliyeguswa mkono kwani ameingiliwa,".

Habari za namna hii sitasita kuzita upuuzi usio na manufaa yoyote kwa wananchi. Mwananchi wa kizazi hiki kinachozidi kubobea kwenye uelewa, hawezi kuendelea kunufaishwa na vijembe au mikwara bubu ambayo haina msaada wowote katika maisha yake.

Wananchi wanataka maji safi si vijembe. Wananchi wanataka kujua mambo ya uchumi, deni la taifa linapaa, hali ya maisha ikoje na mwelekeo wa uchumi wa nchi unakwenda wapi.

Mpigakura makini wa kizazi hiki, anatakiwa kujua sera ya nchi, chama, mwanasiasa au asasi yoyote kuelekea ujenzi wa Tanzania yenye nguvu ya mlo, siyo 'sifa zisizo na maana. Ndiyo maana nasema tuwalazimishe wanasiasa kubadilika.

Tuendako 2025 mwanasiasa asiyetaka kubadilika tumbadilishe .

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Baruapepe; mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# FAHAMU JINSI YA KUTUNZA UAMINIFU WA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

**Mungu alianzisha taasisi hii ili watu waingie, waipende na kuifurahia. Uaminifu katika ndoa huleta furaha, amani na utulivu ndani ya maisha ya wanandoa.**

NDOA ni taasisi ya kijamii yenye maadili yake. Kushindwa kutunza maadili ya ndoa ni kutengeneza mazingira ya mgogoro na kuvunjika kwa ndoa. Jukumu kubwa la wanandoa ni kulea na kutunza maadili ya ndoa.

Mume na mke wanaporidhika kimwili, kihisia, kiakili na kijamii, huwafanya kutokuwa na njaa ya uhusiano mwingine nje ya ndoa. Kunapotokea hali ya kutokuridhika katika ndoa, kunaweza kutengeneza mazingira ya mmoja wa wanandoa au wote kwa pamoja kutafuta njia mbadala za kuziba pengo hilo.

Maisha ni safari ndefu inayohitaji kujifunza na kukua kila siku. Kupata ufahamu mzuri kuhusu uhusiano wa ndoa ni jukumu la maisha yote ya wanandoa. Mtu anapooa au kuolewa afahamu kuwa anaingia katika shule ambayo haina kuhitimu. Hii ni hatua nyingine muhimu ya maisha, hivyo uvumilivu unahitajika sana.

Mungu alianzisha taasisi hii ili watu waingie, waipende na kuifurahia. Uaminifu katika ndoa huleta furaha, amani na utulivu ndani ya maisha ya wanandoa. Katika sehemu ifuatayo nimeeleza baadhi ya mambo muhimu yanayochangia kutunza uaminifu wa ndoa:

- Kuepuka ulaghai hata katika mambo madogo. Ulaghai ndani ya ndoa husababisha kutokuaminiana kwa wanandoa hasa pale ambapo mume au mke anapogundua kuwa alidanganywa katika jambo fulani.

Kutokuaminiana kunapoondoka katika ndoa huleta hisia na mitazamo hasi. Upendo unaondoka na kusababisha karaha kwa sababu siku zote upendo unapoondoka mahali, huondoka na mazuri yake yote.

- Mwenzi ajiepushe kusikiliza maneno ya nje ya nyumba yake na kuyafanyia kazi bila kujiridhisha kuhusu ukweli wake. Ni muhimu kufahamu kuwa, siku zote tunaishi na kutembea na maadui wa ndoa zetu. Kukosa umakini katika eneo hili huweza kuvuruga uhusiano wa wanandoa.

- Kila mwanandoa afanye jitihada za kufanya uhusiano na mwenzi wake kuwa hai na wenye maana. Ndoa huhitaji ubunifu badala ya kuishi kwa mazoea. Kauli nzuri na mawasiliano mazuri, kupeana zawadi, kujali hisia za mwingine, kutendeana mema bila mwenzi kutarajia (surprises) ni kati ya mambo ambayo husaidia kuufanya uhusiano wa ndoa kuwa hai na wenye maana.

- Kuridhishwa katika tendo la ndoa ni jambo muhimu. Tendo la ndoa husimika uhusiano wa wanandoa na kuwaweka karibu zaidi. Tendo la ndoa halipo kwa ajili ya kupata watoto tu, bali lipo ili kuleta furaha katika ndoa, hivyo jitihada za mume na mke zinahitajika ili kufanya tendo la ndoa kuwa la furaha na kuvutia.

- Mume na mke kuishi pamoja na kutengeneza muda wa pamoja ni sehemu muhimu katika kutunza uaminifu wa ndoa. Kitendo cha mume na mke kutokuishi pamoja na kukosa muda wa pamoja, huchangia sana kukosekana kwa uaminifu ndani ya ndoa. Umbali na mazingira ya upweke huchochea baadhi ya wanandoa kuanzisha uhusiano mpya nje ya ndoa ili kuziba pengo la umbali na kuathiri ustawi wa familia.

- Kuboresha hali ya kujali na kuthamini ni jambo la kuzingatiwa. Hakuna mtu anayependa kupuuzwa. Kila mtu anapenda kuonekana ni muhimu na mwenye thamani. Wanandoa wanahitaji kutunzana, kutiana moyo, kusifiana na kupongezana.

Mume au mke afahamu mahitaji yanayogusa hisia za mwenzi wake. Mfano wanaume wanapenda kuheshimiwa, kusifiwa na kutiwa moyo kwa majukumu waliyoyabeba katika familia. Kwa upande mwingine, wanawake wana shauku ya kupendwa, kupongezwa, kusikilizwa na kupokea kauli nzuri kutoka kwa waume zao. Mambo haya pamoja na mengine yasipotekelezwa, huleta hali ya kutoridhika katika ndoa na kutengeneza mazingira ya usaliti ndani ya ndoa.

Ifahamike kwamba ndoa ni taasisi muhimu ya kujenga upendo, amani na mshikamano. Hatuwezi kuwa na taifa imara lenye amani, mshikamano na maadili mema kama ndoa ambazo ni kiini cha familia, jamii na taifa hazitaimarishwa.

Ndoto na matumaini ya kila mmoja wetu wakati anapofunga ndoa, huwa ni kuishi maisha yaliyojaa upendo, furaha na amani tele. Mafunzo haya yanaongeza ufahamu, maarifa na kuwasaidia wanandoa kuishi maisha bora ya ndoa. Endelea kujifunza.

**Dk. Mlyuka ni mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

JUNI 20, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

**Furahia chachandu ya pilipili**



**MAISHA NI NYUMBA**

Namna ya kuchagua fimbo za chuma za kuwekea pazia



**HARUSI**

Ukurasa 12





**NYWELE FUPI**

# Urembo wenye faida nyingi kwa mwanamke

Ukurasa 14

## MAJIBU








| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| T | U | N | G | U | A |
| A | ■ | ■ | ■ | M | ■ |
| A | G | A | ■ | M | ■ |
| ■ | O | ■ | B | A | A |
| ■ | L | ■ | ■ | ■ | P |
| S | I | L | I | B | A |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5





## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
ARI, SAA, KAA, AYA,
ROZI, RAIA, SIMIKA, KIFARU

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

UNGEKUWA wewe ni mwalimu ungemfanyaje mtoto huyu?

**Mwalimu:** Punda ni mnyama anaefugwa nyumbani,lakini akiwa mwituni anaitwa pundamilia, je, sungura anayeishi mwituni anaitwaje?"

**Mwanafunzi:** "Sunguramilia."

**Mwalimu:** Rais wa kwanza wa kenya aliitwa Kenyatta, je, rais wa kwanza wa Tanzania aliitwaje?"

**Mwanafunzi:** "Tanzaniatta"

**Mwalumu:** "Kuku yuko katika jamii ya ndege, je, samaki yuko katika jamii ya nini?"

**Mwanafunzi:** Meli

**Mwalimu:** Wee kweli zuzu

**SWALI**

Vyakula gani ni jamii ya wanga?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Upendo unavyobadili maisha ya ndoa iliyovurugika

KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo nijadili roho ya upendo inavyoweza kubadili maisha na hasa ndoa zilizojaa sintofahamu nyingi.

Mungu mara zote katika maandiko yake anasisitiza watu kuwa na upendo kwa kuwa yeye mwenyewe ni pendo. Hiyo ni amri yake kuu kwamba tupendane kama yeye anavyotupenda. Upendo ni nguvu hivyo yatupasa kuenenda katika upendo siku zote. Tafsiri nyingine ya upendo ni sadaka na dhabihu.

Kinachobadilisha maisha ya mtu ni upendo. Hakuna nguvu nyingine yoyote inayoweza kubadilisha mume au mke wako, rafiki yako kama nguvu ya upendo.

Hebu mpenzi msomaji nikupe ushuhuda huu uone jinsi upendo ulivyo na nguvu ya kubadilisha tabia iliyokuwa mbaya na kuwa nzuri hata kushangaza wengi. Kile kilichoonekana kuwa hakiwezekani, sasa kimekuwa tumaini jipya katika maisha.

Mama mmoja aliolewa na mume ambaye kabla yake alishaoa na kuacha wanawake watatu. Mume huyu ambaye pamoja na kuteswa na roho ya mitala(kuoa wake wengi), alikuwa pia mlevi wa kupindukia. Akishalewa alikuwa akibebwa na wenzake kumrudisha nyumbani kwake akiwa chakari.

Sasa huyu mama ambaye ni mke wa nne akafanya kitu cha ajabu sana kwa baba huyu hadi ndugu na majirani zake wakafikia hatua kusema kuwa amemroga mumewe.

Wakwe zake nao pia wakasema, "kama kuna mwanamke mchawi, ni huyu!" Uchawi unaozungumziwa ni pale huyo mwanaume alipoacha pombe baada yeye kuolewa katika mji huo.

Kilichowaacha midomo wazi ni pale mume alipoacha pombe wakajenga nyumba nne, jambo ambalo halijawahi kutokea katika historia ya mwanamume huyo. Fedha zake zilikuwa zinaishia kwenye ulevi na michepuko mbalimbali.

Lakini baada ya kumpata mama huyo wa nne, nyumba zikajengwa, magari yakanunuliwa na mume akaacha pombe kabisa. Kule kutamkwa kwamba mama huyu ni mchawi kulitokana na kumbadilisha mume wake.

Yule mama akaulizwa swali; Je, uliendа kwa mganga gani kumbadilisha huyu mwanamume aliyekuwa na kiburi namna hii na akaacha pombe? Akajibu kwa kusema;

"Mimi nilipoamua kuolewa na huyu baba, niliamua kuvaa viatu vyake. Nilijua ana shida gani, nikatumia upendo. Vituko vyote alivyokuwa akivifanya, mimi nilimuonyesha upendo. Nilikuwa sijali mambo anayofanya hivyo nilijishusha mpaka mahali alipo.

Mpenzi msomaji, mama huyu ilibidi ashuke aenende na hali yake, akakubali kufanana naye. Huo ni upendo. Huwezi kumbadilisha mtu kama wewe unajifanya kuwa bora kuliko yeye.

Hata tukirudi nyuma pale mahusiano yanapoanza, tamko kuu linalotawala ni upendo. Mwanamume huanza kumwambia mwanamke, "nakupenda uwe wangu", naye hujibu "nakupenda pia".

Mwanamke akiamua kumpenda mwanamume hupenda hasa, lakini akimchukia, ndio hivyo tena. Kwa mama niliyemjadili hapo juu, alimpenda mumewe hakuangalia udhaifu wake, alimpenda jumla, hatimaye akapata mafanikio.

Huyo ni mwanamke anayejitambua yeye ni nani kwa mumewe. Mungu alimuumba mwanamke awe msaidizi wa mwanamume. Msaidizi kwa lugha ya Kiebrania ni; mtu wa kuongozana naye (kuambatana), ni ngao, mlinzi na mtetezi.

Mama huyu, mke wa nne, hakika alitambua ndani yake kwamba ili kuleta maelewano na maendeleo ndani ya ndoa yake, alipaswa kuwa na roho ya ujasiri na uvumilivu. Mwanamke kama ngao ya mwanamume, siku zote atashambuliwa na shetani kwa kumletea kila aina ya matatizo.

Shetani alifanikiwa kuwashambulia kinamama wale waliotangulia kwa sababu alijua kuwa yapo mafanikio makubwa mbele ya mwanamume yule. Hata hivyo, bahati ya kufaidi mafanikio hayo ikaangukia kwa mke wa nne ambapo Mungu alimpa ufunuo wa upendo, nao wote wakafanikiwa. Hiyo ni siri iliyokuwa imejificha.

Ulevi na vituko vingine ndivyo vilivyomtawala mwanamume yule hadi wake zake wakaona ni kero. Lakini mke wa nne alisimama kidete kushinda roho zinazomtesa mumewe kwa kutumia silaha ya upendo.

Alitumia maneno ya upole na utii kumrejesha mwanamume huyo katika anga la upendo wa kwanza hatimaye akafanikiwa. Siku zote yatupasa kumshirikisha Mungu pale tunapopita katika nyakati ngumu.

***Unapoona mambo ni magumu sana, usiogope kwani muujiza wako upo mbele yako. Maisha Ndivyo Yalivyo! Kwa leo naishia hapa. Je, una maoni, kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Taa hizi za barabarani zinatumika kuumiza madereva

UNAPOENDESHA gari kuelekea Posta kutokea Kinondoni-Morocco, lazima upite kwenye taa sita ambazo zote lazima ufuate utaratibu wa kusimama na zikishakuruhusu ndipo uendelee na safari yako.

Taa hizo ni za Morocco ambako kuna matengenezo ya barabara yanayoendelea na mara nyingi kuna askari wa usalama barabarani wanaoongoza magari, lakini mara chache taa zinatumika.

Ukishavuka taa hizo kuna taa za Namanga ambazo kama ilivyo kawaida ni lazima usimame na baadaye uruhusiwe ndipo uendelee na safari.

Ukisogea mbele kuna taa za Mbuyuni ambazo kama iliyo kawaida ya sheria za usalama barabarani, lazima usimame tena ikishakuruhusu ndipo uendelee na safari. Ukiendelea na safari utakutana tena na taa za Ubalozi na mbele kuna taa za Selander na zingine za Serena. Zote hizo zimechakaa kiasi cha kuwa mtaji kwa askari wa usalama barabarani.

Kati ya zote, zilizo taabani zaidi ni za Namanga na Mbuyuni ambazo wakati mwingine huwasha taa ya njano wakati inatakiwa kuwa kijani, ili kuruhusu magari kupita, jambo ambalo linawachanganya madereva.

Pia taa inayoruhusu magari kuelekea Msasani haiwaki inatumika nyingine na ikiwa dereva atapita basi polisi huwa wamejificha eneo fulani kwa ajili ya kukamata magari kwa madai yamepita kwenye taa nyekundu.

Nyingine ni za Mbuyuni. Ukiwa unatokea Posta, nazo huwaka njano wakati inatakiwa kuwa kijani na wakati mwingine haieleweki na dereva akipita basi hujikuta mikononi mwa polisi ambao hujificha chini ya mti.

Kwa jumla taa zote nilizozitaja ni maumivu kwa madereva na imekuwa sehemu ya askari kukamata madereva kwa makosa ya usalama barabarani kwamba wamepita kwenye taa nyekundu. Jambo hilo ni maumivu kwa madereva kutokana na kutozwa faini kwa makosa ambayo kimsingi hayapo.

Kutokana na taa hizi kuwa katika hali hiyo, kuna uwezekano mkubwa wa ajali kutokea kwa kuwa dereva ataona taa imemruhusu kumbe kiuhalisia haiko hivyo na wakati mwingine magari kukutana eneo moja.

Lakini kubwa ni ubishani ambao hujitokeza baina ya askari ambao wakati mwingine wanajua wazi matatizo ya taa hizo na kumtaka dereva kutumia taa zingine za mbele yake wakati huo alitaka kwenda kulia.

Askari wanachofanya katika eneo la Namanga ni kusimamisha magari yote ya mwisho kwenye kila kundi lililopita na utakuta ni magari matatu au mawili na wote wanaambiwa wanakabiliwa na kosa la kupita kwenye taa nyekundu na ukibisha wanatishia kukupandisha mahakamani.

Kinachozua maswali na wasiwasi ni kuwa askari hao wanajua taa hizo haziko sawa, kilichotarajiwa ni kuhakikisha marekebisho yanafanyika ili madereva wawezi kupita kwa kuzingatia sheria.

> **“Yako maeneo yenye kicheko hasa kwenye makosa ya usalama barabarani kwa bajaji na bodaboda na bidhaa za zinazozalishwa nchini kama za ujenzi ambazo zinatumiwa na wananchi wengi.**

Ni vyema Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) wakafanya ukaguzi wa kina wa taa hizo ili kujiridhisha kama zinafanya kazi inavyotakiwa na kama zinahitaji kuondolewa, kurekebishwa au kusafishwa ikafanyika hivyo mapema.


Taa hizi ambazo baadhi zinafanya kazi unakuta zimefifia kiasi ambacho wakati mwingine dereva anaweza asione vizuri kuwa ameruhusiwa au kuzuiwa au anatakiwa kuajiandaa kuondoka.

Badala ya taa sasa kutumika kama fimbo kwa madereva wengi ni muhimu polisi wakawajulisha TANROADS kuhusu ubovu huo ili zirekebishwe na kuondoa lawama za kutoza faini umiza.

Pia kama wanaona taa hizo zimepitwa na wakati basi ni muhimu ziwekwe taa mpya zenye kuhesabu dakika kama maeneo mengine ili kuhakikisha dereva anaona dakika na kama akipita basi atakuwa amefanya kusudi.

Mungu ibariki Tanzania.


# HARUSI












Shangwe na nderemo zilitawala katika familia ya Bwana na Bibi Kakokere baada ya binti yao Beatrice Kakokere, kufunga ndoa na Wilfred Mworia katika Kanisa la Katoliki la Mtakatifu Peter Juni 5, mwaka huu. Kabla kulifanyika sherehe ya aina yake ya kumpongeza katika ukumbi wa Masiani uliopo Mbezi Beach jijini Dar es Salaam.





# MITINDO





KHADIJA MWANAMBOKA

## Miaka 25 ya machozi, kicheko kwenye mitindo

MWANAMITINDO maarufu nchini Khadija Mwanamboka,wiki iliyopita ametimiza miaka 25 katika tasnia ya ubunifu na kueleza safari hiyo kwake ilikuwa ya maumivu na kukatisha tamaa.

Katika sherehe hiyo ambayo iliambatana na jukwaa la mavazi kwa watoto, ilihudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Sanaa na Michezo, Abdallah Posi, pamoja na mastaa mbalimbali wa mitindo.

Akizungumza na Nipashe, Mwanamboka amesema alipoanza kwa mara ya kwanza ndoto yake ilikuwa ngumu kutimia kutokana na vikwazo alivyokutana navyo.

Amesema changamoto alizokabiliana nazo kutokana na fani ya ubunifu kutokuwa na wafadhili na uwanja mpana wa kujulikana na Watanzania wengi.

Khadija amesema kipindi cha nyuma ilikuwa vigumu wabunifu kufahamika kutokana na vyombo vya habari kuwa vichache, na vingi havikuona umuhimu wa kutangaza fani hiyo kama ilivyo sasa.

"Nakumbuka zamani ilikuwa vigumu kupata matangazo, nilitembea na Albamu ya picha kwenda kwa watu mbalimbali kuonyesha kazi zangu, magazeti na hata redio ilikuwa nadra kutoa taarifa," amesema Khadija.

Ameeleza kwa sasa imekuwa rahisi kuonekana, lakini bado imekuwa kazi ngumu kupanuka kutokana na serikali kutoweka njia nzuri ya kupata wafadhili kama ilivyo katika sanaa nyingine.

"Wakati umefika sasa serikali kuweka mikono yake yote katika fani ya ubunifu ili tuwe kama sanaa nyingine katika kupata ufadhili na uwanja mpana wa kuonyesha kazi zetu," ameongeza kusema.

Mbunifu huyo wa mavazi, amesema ndoto yake kubwa ni kueneza ujuzi huo maeneo mengi nchini Tanzania, tayari ameanzisha mchakato wa kununua basi litakalotumika kutafuta vipaji vipya vijijini.

Ameomba serikali, taasisi binafsi na watu mbalimbali kumsaidia kwa kuchangia mradi huo ambao ukifanikiwa ataweza kuwafikia vijana wengi nchini.

Khadija anajivunia kuwa chemchem iliyowaibua wabunifu maarufu wanaotamba kwa sasa kama Mustafa Asanali na Ally Remtula.

Hata hivyo, Posi alimhakikishia serikali kumuunga mkono katika miradi yoyote itakayokuza sanaa hiyo, lakini ni muhimu kuungana na wabunifu wengine ili iwe rahisi kuwanufaisha kwa pamoja.



URBEMBO

NYWELE FUPI

# Urembo wenye faida nyingi kwa mwanamke

KILA mwanamke huchagua aina gani ya nywele anazotaka ili kuonekana maridadi, mwenye mvuto na anayekwenda na muda.

Kuna wanaotengeneza nywele zao kwa kuziweka zile za bandia, kusuka au kuzichana na kuzifunga kwa banio.

Hata hivyo, mtindo wa kukata nywele unaweza kuwa bora zaidi kutokana na kuongeza mng'aro wa mwonekano wa mtu husika hasa kutokana na kuwa chaguo la aina nyingi ya ukataji.

Nywele ndefu haikubaliki kwa kila mtu, hivyo harufu nzuri za nywele za kike ni njia ya nje kwa wale ambao wanataka kuangalia umaridadi, kawaida na hata ubunifu.

Ukataji wa nywele kwa mwanamke unaweza kumfufua, kubadilisha taswira yake na kumsababishia ushawishi kwa watu wengine kutokana na mwonekano wake.

Hata hivyo, utunzaji wa nywele fupi hauna gharama kubwa, hivyo ni rahisi kwa mwanamke kuelekeza nguvu ya kifedha katika mambo mengine ya maendeleo.

**NAMNA YA UTUNZAJI**

Ni tofauti na aina nyingine za nywele, kwani utunzaji wake ni rahisi na unampa mtu uamuzi wa kuweka mitindo katika muda mfupi. Jambo la kuzingatia ni kulisha nywele vizuri.

Unaweza kusafisha nywele kwa shampoo au maji ya vuguvugu yenye mchanganyiko wa viungo vya asili vinavyotunza nywele kama parachichi na mafuta ya nazi.

Kukata nywele ni sawa na kuzipumzisha kutoka mtindo mmoja hadi mwingine hali ambayo inasababisha tezi za sebaceous za kichwani kuzidiwa na mafuta mengi ya ziada, ambayo yanaweza kuathiri hali ya nje na kuathiri ubora wa nywele.

Mara nyingi wanawake wanaokata nywele hufanya sura zao kuwa laini zaidi kutokana na mishipa inayopita kichwani kutosumbuliwa na joto kali la mashine za kulainisha nywele au dawa kali zinazounguza vioteo kichwani.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia chachandu ya pilipili





PILIPILI ni kiungo kinachompa mlaji hamu ya kula chakula, inaweza kuwekwa kwenye chakula chochote mlaji anachopendelea ili kuongeza ladha .

**MAHITAJI**

Karoti tatu kubwa, pilipili hoho moja, vitunguu swaumu, vitunguu maji vitano, tangawizi, majani ya giligiliani na ndimu.

Mahitaji mengine ni chumvi, mafuta ya kula kidogo, pilipili mbuzi tatu au utakavyopenda, nyanya 3 zilizoiva vizuri.

**MAANDALIZI**

Menya nyanya, hoho, karoti ,vitunguu maji ,vitunguu swaumu, tangawizi na majani ya giligiliani yachambuliwe.

Kata kata vitunguu maji na nyanya weka bakuli tofauti, twanga vitunguu swaumu na majani ya giligiliani, kwangua karoti pia katakata pilipili hoho.

**NAMNA YA KUPIKA**

Bandika mafuta jikoni, yakipata moto weka vitunguu maji koroga dakika mbili, weka vitunguu swaumu na giligiliani koroga tia tangawizi kisha hoho na karoti.

Acha kidogo kisha weka nyanya, kamulia ndimu tia chumvi funika mpaka nyanya iive vizuri na katia pilipili zako dakika tano baada ya kuweka pilipili epua iache ipoe.

Ukiona imepoa iweke kwenye brenda isage hapo pilipili yako itakua tayari kwa kujilamba.

MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Zijue athari za kuokoteza ramani za nyumba

## Dondoo ya kuchagua fimbo za chuma za kuwekea pazia




**1:** Chagua fimbo yenye ukubwa kupita dirisha lako ili unapoweka pazia lifunike uwazi wote. Fimbo ukiwa kubwa pia inapendezesha dirisha.

**2;** Chagua chuma chenye ubora na ikiwezekana kiwe na mchanganyiko wa Alluminium kwa ajili ya kukifanya kiwe chepesi pale kinapowekwa juu ya dirisha.

**3:** Ni muhimu kuchagua mapambo mazuri yanayowekwa kila ncha ya chuma, kwani ni sehemu ya kupendezesha dirisha.

**4:** Rangi ya chuma ni vizuri ikaendana na mapazia unayoyaweka ili kuongeza nakshi ndani ya nyumba yako.



UJENZI wa nyumba hauwezi kufanyika pasipo kuwapo na ramani inayoonyesha dira ya aina ya nyumba inayotakiwa kujengwa.

Pamoja na kutakiwa kuwapo kwa ramani kabla ujenzi wa nyumba, wako baadhi ambao hawalichukulii kwa umakini suala la kuwa na ramani kutoka kwa wataalam wanaoeleweka na badala yake 'kuokoteza' tu.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Lameck Kashabo, anasema kuokoteza ramani na kutokuthamini kile unachokwenda kujenga licha ya kwamba unatumia mamilioni ya pesa kujenga ni hatari na mwisho wake ni majuto.

"Inashangaza sana kwamba unakuta mtu anaenda kujenga nyumba ya Sh. milioni 90 lakini anaokoteza ramani kutoka kwa wasio wataalam au anatafuta ramani ambayo imetumiwa na mtu mwingine wakati gharama ya kumtumia mtaalamu kwa huduma yote ya ushauri pamoja na michoro labda ni Sh.600,000 ambayo haifiki hata asilimia moja ya gharama yote ya ujenzi. Maamuzi (uamuzi) ya (wa) aina hii kwa vyovyote vile yanaambatana na hasara kubwa na majuto ya baadae," anasema Kashabo.





"Madhara ya kuokoteza ramani ya nyumba kisha ukaijenga, iwe ni kutoka kwenye mitandao au ni kutoka kwa mafundi wa mitaani au kwa namna nyingine yoyote ile ni kushindwa kuithamini nyumba unayotaka kujenga licha ya kwamba unakwenda kutumia pesa nyingi sana kujenga," anasisitiza.

Anasema miongoni mwa madhara ya kuokoteza ramani ni kushindwa kupata aina ya nyumba unayotaka kwa kulazimika kukubaliana na chochote unachokutana nacho kwenye ramani unayookoteza.


"Kila mtu huwa na vipaumbele tofauti na vya mwingine, karibu kila kazi tunayokutana nayo huwa ni vigumu kufanana na ya mtu mwingine kwa vipaumbele vya kimahitaji, achilia mbali utofauti wa ukubwa wa viwanja, utamaduni na mengineyo, ndiyo maana huwa nawashauri watu kufanya kitu kinachoendana na vipaumbele vyao.

"Huwezi kufurahia nyumba ambayo siyo chaguo lako, hata kama ikitokea ukapenda aina fulani ya jengo au nyumba kutokana na muundo wake, bado kwa ndani kuna vitu hutavifurahia namna vilivyopangika.

"Unachotakiwa ni kuchukua picha ya lile jengo ulilolipenda na kisha kumwonyesha mtaalamu, kumwambia kwamba nataka liwe na mwonekano huu lakini ukamwelekeza alipangilie upya kwa ndani na mwisho wa siku libaki na muonekano ule unaoupenda wewe.

"Unaweza kujuta sana baadae unapookoteza ramani, kisha ikajengwa kama ilivyo au hata kama itabadilishwa ikawa kienyeji sana na hata usiipende tena. Bila kutumia utaalamu sahihi mara nyingi changamoto zake unakuja kukutana nazo baada ya kuanza kuitumia," anasema.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
NATUPIWA MACHO MPAKA NAISHI KWA 'MASHAKA'
'UMEHAMIA KABISA?
UNAROPOKA SANA UKIONA WAGENI, KWANI TABIA HII UMEITOA WAPI?
'KWAKO...
'ANADAI TALAKA KWA VURUGU MBINDE NA MIT#S! UKIJARIBU KUTOA 'UNAULIZWA UNA-MPA NANI?'
HAKUNA WA KUNI-NYAMAZISHA HUMU!!! MIMI NAJUA HAKI YANGU KAMA ABIRIA
FUNGA DOMO LAKO BHANA! UNAJIJUA UMEAMKA NAYO UNATUHUBIRIA...
KWANI KALIPA SHILINGI NGAPI ARUDISHIWE ASHUKE TUPATE HEWA...!
HAKUNA HAKI YA KUPOTOSHA ABIRIA WENZAKO KWA SABABU KUONGEA KILEVILEVI NI KUTUPIGIA MIKELELE!
ACHA HIZO! UNGETAKA HEWA BAJAJI ZIPO KIBAO! LAKINI UPO HUMU TULIA KAMA MOJA!
UKILITAZAMA KWA MACHO KABLA HUJAJITWISHA 'NI JIPESIIIII'
UONGO-DHII
BIA YA NANE HIYO MWANAMKE MKAVU KAMA UNAKUNYWA TOGWA!
MWENZAKO JANA 'KRETI NNE' SIGARA SITINI LAKINI HAJANI-SIMANGA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...JIKO LA MBEA HALIKAWII KUUNGUZA

HABARI KIMATAIFA

# Tshisekedi aweka kando mazungumzo na ADF

**Kinshasa,** DRC

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Thisekedi ameendelea na ziara yake Mashariki mwa nchi hiyo, akisema hakuna uwezekano wa kujadiliana na kundi la waasi la ADF.

Kundi hilo limeendelea kutekeleza mauaji ya raia. Jana, kiongozi huyo alitarajiwa kuwa mjini Bunia, katika ziara ya kutathmini hali ya usalama katika eneo hilo.

Rais alipokea wawakilishi wa tabaka mbalimbali za kijamii, ili kupokea maelezo juu ya mapendekezo yao kufanikisha mapambano na makundi ya waasi yanayotekeleza mashambulizi yanayolenga raia kwa kiasi kikubwa

Mwaakilishi wa jamii ya kiislamu katika eneo hilo, Cheikh Umudi Bakari alisema:

"Kulingana na hali ya uislam, tume yatakiwa aweze kujitetea, namna alivyofanya mwenzake Joseph Kabila alipokuwa hapa ziarani, kusema kwamba waislam ambao wako Mjini ni raïa, Tunajua kuwa siku za usoni ataweza kuzungumza mambo kama haya, kuonyesha utofauti raia na walio katika vikundi vya wapiganaji, sababu uislam hauwezi kuruhusu ukatili namna inavyofanyika hapa katika mji wetu."

Mwaka jana zaidi ya raia 1,300 waliuawa kikatili na watuhumiwa waasi wa Uganda, ADF, Mashariki mwa Congo.

**RFI**

# Wanafunzi 80, walimu watekwa Nigeria

**Kebbi,** NIGERIA

WATU wenye silaha wamemuua afisa mmoja wa polisi na kuwateka nyara wanafunzi 80 na walimu watano kwenye shule ya jimbo la Nigeria la Kebbi, ripoti ya Shirika la habari la Reuters, imesema ikinukuu polisi na wakazi wa jimbo hilo.

Hilo ni shambulizi la tatu la utekaji nyara wa watu wengi katika kipindi cha wiki tatu, Kaskazini mwa Nigeria, viongozi wakisema vitendo hivyo vya utekaji nyara vinafanywa na majambazi wenye silaha wanaodai fidia.

Usman Aliyu, mwalimu kwenye shule iliyoshambuliwa, alisema watu hao wenye silaha wamewachukua wanafunzi 80 wengi wao wakiwa wasichana.

Msemji wa polisi katika jimbo la Kebbi Nafiu Abubakar alisema watu wenye silaha walimuua afisa wa polisi na kumpiga risasi mwanafunzi ambaye anapatiwa matibabu.

Hadi mwishoni mwa wiki, polisi walikuwa hawajatangaza idadi kamili ya wanafunzi waliotekwa nyara. Shambulizi lilifanyika kwenye chuo kikuu cha serikali katika mji ulio mbali wa Birnin Yauri.

Msemaji wa Polisi katika jimbo la Kebbi Abubakar alisema maofisa wa usalama wanawatafuta wanafunzi na walimu waliotekwa nyara katika msitu ulio karibu.

**VOA**

# Museveni atangaza masharti kutotoka nje

**Kampala,** UGANDA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ametangaza kutotoka nje 'lockdown' ikiwa ni masharti mapya ya kupambana na ongezeko la visa vya virusi vya corona.

Hatua hizo zilianza kutekelezwa juzi baada ya kutoa hotuba kupitia televisheni akisema kuwa usafiri wote wa kibinafsi na wa umma umepigwa marufuku kwa siku 42 zijazo, isipokuwa kwa huduma muhimu na mizigo.

Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Entebbe na vivuko vingine vya mpaka wa ardhi hata hivyo vitabaki wazi kwa watalii na wale wanaorejea, ingawa mamlaka zilipewa jukumu la kuhakikisha kuwa hakuna kesi mpya za Covid-19.

Amri ya kutotoka nje, ilianza saa tatu usiku hadi alfajiri na kwamba waendeshaji pikipiki, wanaojulikana kama bodaboda wanaruhusiwa kubeba bidhaa tu.

Kazi zote zinazozingatiwa sio za lazima, shule na taasisi za kujifunzia, sehemu za ibada na hafla za michezo pia zimefungwa kwa siku 42 zijazo.

Vituo vya biashara na maeneo ya biashara pia yamefungwa na wachuuzi wa soko wakiruhusiwa kulala kwenye vibanda vyao.

Masharti ya sasa ni sawa na ya Machi mwaka jana, wakati nchi nzima ilipofungwa kabisa.

Rais Museveni alisema hatua hizo ni muhimu kukomesha maambukizi ya sasa ya kijamii na kupeuka kuuelemea kabisa mfumo wa utoaji wa huduma za afya.

Katika siku 12 zilizopita, nchi hiyo ilirekodi vifo 190 vinavyotokana na corona.

Rais alionya kuwa kwa kiwango hicho cha maambukizi, mahitaji ya oksijeni katika vituo vya afya yangeongezeka mara tisa na nchi haiwezi kukabiliana na hali kama hiyo.

Rais pia aliamuru wahudumu wa baa na vilabu vya usiku, wakipuuza sheria za kufungwa wapokonywe leseni za kuhudumu.

Baa na sehemu za burudani zilifungwa rasmi Machi, mwaka jana, zingine zimekuwa zikifanya kazi kinyume cha sheria.

Na kwamba watakaopatikana wakihudumia wateja watakamatwa na kutakiwa kulipa faini kubwa.

Idara za serikali zitakuwa na asilimia 10 tu ya wafanyakazi wao wanaofanya kazi kutoka ofisini.

Tangu mwishoni mwa Mei, mwaka huu wakati nchi ikiwa na wimbi la pili, visa vya corona vimekuwa vikiongezeka haraka.

Katika mji mkuu Kampala, zaidi ya visa 15,300 vimerikodiwa katika siku ishirini na moja zilizopita na jumla ya visa 9,000 hurekodiwa kila wiki nchi nzima.

Kiwango cha maambukizi kikiwa asilimia 17, Rais Museveni alisema anahofia idadi halisi ya visa na vifo kuwa kubwa zaidi, watu wengine kuugua na kufa katika jamii zao bila kutafuta huduma au hata katika vituo vidogo vya afya na upimaji haupatikani.

Uganda ina zaidi ya vitanda 3,700, kuvishughulikia visa vya corona katika vituo vya afya vya umma na vya kibinafsi.

**BBC**



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, akilihutubia Baraza Kuu la UN (UNGA), baada ya kuchaguliwa tena kushika nafasi hiyo kwa muhula wa pili, kwa kipindi cha miaka mitano, jijini New York, Marekani, juzi. Muhula wake wa pili unaanza rasmi Januari Mosi, mwakani. **PICHA: XINHUA**

# Ethiopia yajiandaa kwa uchaguzi

**Addis Ababa,** ETHIOPIA

ETHIOPIA inajiandaa kwa ajili ya uchaguzi wa bunge unaofanyika Jumatau wiki ijayo, chama kitakachoshinda kitaunda serikali kwa kutoa waziri mkuu.

Serikali ya sasa inayoongozwa na Waziri Mkuu Abiy Ahmed, imeahidi uchaguzi huo utakuwa huru na wa haki, ingawa matatizo kadhaa yatawazuia wananchi wengine kupiga kura.

Tume ya Uchaguzi ya Ethiopia, ilisema imeweka mikakati ya kutosha kuhakikisha kuwa wananchi watakaopiga kura watafanya hivyo kwa njia halali na huru. Kulingana na tume hiyo, zaidi ya wananchi milioni 37 wamejisalili katika maeneo mbalimbali ya nchi. Hata hivyo, kati ya majimbo 547, majimbo 110 hayataweza kushiriki katika uchaguzi.

Tume ya uchaguzi ilisema kuwa maeneo mengine hayawezi kufikiwa kwa sababu ya ukosefu wa usalama na mengine kwa ajili ya miundombinu duni na sababu ambazo haziwezi ruhusu vituo vya kupigia kura kuwekwa huko.

Kwa hivyo kutakuwa na awamu ya pili ya uchaguzi, yumkini katika mwezi Septemba, kwenye maeneo hayo, likiwamo Jimbo la Kaskazini la Tigray, ambako vita baina ya jeshi la serikali kuu na la jimbo hilo vimempaka matope.

Umoja wa Mataifa (UN), ulisema zaidi ya watu milioni tano kwenye jimbo hilo wako katika hali mbaya na zaidi ya milioni moja, wamelazimika kuyakimbia makazi yao.

Eneo zima la Kaskazini linasemekana kuwa linahitaji usaidizi wa haraka. Zaidi ya wananchi milioni 37 wamejisalili katika maeneo mbalimbali ya nchi

**DW**

MAKALA

# BARUA YA WAZI KWA RAIS KUHUSU NHIF



Na Magabilo Masambu

> Iko hoja kwamba masuala ya bima ukichangia si lazima unufaike wewe na kwamba unachangia wasiojiweza. Hivi inaingia akilini kwamba wasiojiweza wapo ndani mwako sheria haiwanufaishi, lakini unachangia watu wengine usiowajua. Kama uzalendo ndiyo huo..

NDUGU Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naandika barua hii kwako kwa unyenyekevu mkubwa nikiamini kwamba kwa mamlaka uliyo nayo kwa mujibu wa sheria, utatoa suluhu ya tatizo binafsi ninalofikiri ni tatizo la wengi.

Mheshimiwa Rais, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ni mpango wa bima ya afya wa kisheria ulioanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 8 ya mwaka 1999 ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za afya kwa wanachama na wategemezi wao.

Uanachama huo ni kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya Sura ya 395 Toleo la mwaka 2015 na kanuni zake za mwaka 2002. Katika sheria na kanuni hizo imeweka mipaka ya wanaotakiwa kunufaika na mpango huu. Wanaotajwa ni mchangiaji mwenyewe na mwenza wake, watoto wa kuwazaa, kuasili au kufikia, wazazi wa mchangiaji au wakwe zake.

Sina tatizo na sheria kwa sababu ni mawazo ya watu. Walikaa wakapanga utaratibu uwe hivyo na ukapitishwa ikawa sheria. Si vibaya mawazo yangu haya yakakubaliwa, kupitishwa na mwishowe yakawa sheria vile vile.

Ndugu Rais, kilichonisukuma nikuandikie barua hii ni jambo la mchangiaji kupangiwa wategemezi. Tatizo haliko kwenye idadi, inaweza kubaki hiyo ya watu sita kama ilivyo sasa lakini sheria isitamke kwamba ni nani na nani wanaotakiwa kuwa kwenye mpango huo. Mchangiaji awe huru kuweka mtegemezi anayemtaka na sababu zake ni kama ifuatavyo;- Moja, kuna wachangiaji ambao hawana watoto wa kuwazaa kwa sababu yoyote ile. Mbaya zaidi waneweza kuwa pia hawana wazazi lakini watumishi hao wanalea wadogo zao wa kuzaliwa pamoja, watoto wa ndugu ambao wengine wazazi wao wamefariki dunia, bibi zao na wanafamilia wengine ambao wanawategemea kwa asilimia 100 kama wazazi wao.

Nafahamu kuna kipengele cha kuasili, lakini ukweli ni kwamba taratibu za kuasili ni ngumu sana pia kuna wategemezi ambao kwa mujibu wa sheria huwezi kuasili na wanakutegemea kwa asilimia zote.

Pili, kuna kundi lingine la watumishi wana watoto lakini pia wameachiwa familia na ndugu au wazazi wao waliofariki dunia. Mathalani, kwenye familia X mtumishi Y ni mtoto wa kwanza kwenye familia, wazazi wao wamefariki dunia amebaki analea wadogo zake ambao hawana usaidizi wowote zaidi yake lakini Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya haiwatambui. Kwa hiyo unakuta mtumishi Y anakatwa fedha kila mwezi za uanachama, anatibiwa yeye na kama ameoa na mwenza wake huku akitoa tena fedha nyingi mfukoni kuwatibia nduguze. Unajaribu kujiuliza hivi mfuko wa bima ya afya unamaana gani kwa mtumishi? Ni suala la kuleta nafuu kwa mtumishi au ni suala la kuchangia tu na kama ni kuchangia kwa nini lisiwe la kila mtu ndani ya nchi?

Iko hoja kwamba masuala ya bima ukichangia si lazima unufaike wewe na kwamba unachangia wasiojiweza. Hivi inaingia akilini kwamba wasiojiweza wapo ndani mwako sheria haiwanufaishi, lakini unachangia watu wengine usiowajua. Kama uzalendo ndiyo huo, kwa nini ni kwa watumishi wa sekta iliyo rasmi pekee hasa watumishi wa umma kama walimu na wauguzi?

Kuna uwezekano mkubwa waliopitisha sheria hii haya hayawahusu kwa sababu ama ya kuwa na mishahara mikubwa kwa hiyo hawaoni tabu ndugu zao wanapougua kwenda kugharamikia kwa fedha za mfukoni au pengine bima zao zimewapa uhuru wa kumtibu yeyote kwenye familia. Jambo hili linawaumiza sana watumishi wa umma ambao wengi wana mishahara midogo, wasio na marupurupu kama ya wabunge. Wengi wao wana wategemezi wengi kutokana na kwamba wanatoka katika familia za kawaida sana.

Ni ukweli kwamba idadi ya watu sita ni ndogo kutokana na aina ya familia zetu za kiafrika. Ukweli kwamba kila mtu kwenye familia hawezi kutibiwa na bima ya afya unajulikana, lakini idadi hiyo ndogo ya watu sita sheria isitaje nani anatakiwa. Suala la msingi ni kuzingatia idadi ila mtumishi aamuwe vinginevyo bima hii itakuwa haina lengo la kumpa nafuu mtumishi badala yake itakuwa janja ya kuchukua fedha zake ili kuwalipa mishahara mikubwa watumishi wa mfuko na kufanyia mambo mengine ambayo yako nje ya utaratibu wa huduma ya afya.

Iko hoja kwamba tukiwaruhusu wawe huru wataweka watu ambao si ndugu zao, kwani hata wakiweka watu ambao si ndugu zao watu hao si Watanzania? Kama lengo ni kuchangia huduma za Watanzania wasiojiweza, kuna shida gani hata ikitokea hivyo?

Kama hesabu zilipigwa kwamba kwa makato haya wanaostahili kupata huduma ni sita kuna shida gani kila mtumishi akiwa na wategemezi wote sita au kama mfuko unatumia sheria kujinufaisha kwa sababu kwa sheria jinsi ilivyo inawazuia watumishi wengi wasiwe na wategemezi sasa kama lengo litakuwa hilo basi watumishi wanaibiwa fedha zao.

Kwa barua hii Ndugu Rais, nakuomba sana uone uwezekano wa kuagiza mamlaka zinazohusika, kufanya marekebisho ya sheria hii ili kuwapa uhuru watumishi maana ndio wanaofahamu nani mhitaji zaidi katika familia ili kupunguza magojwa ya kisukari na presha kwa watumishi wanaotegemewa. Kwa kweli magonjwa mengi husababishwa na kuwaza namna ya kutatua shida za familia hasa matatizo ya ugojwa ambayo hayapigi hodi.

Mwisho nikutakie kazi njema. Watanzania tuna imani na wewe, tutaendelea kukushauri yale tunayoona kwamba yanapaswa kukaa sawa kupitia kalamu zetu ili kuhakikisha kila Mtanzania anajivunia kuishi kwenye nchi yake kama mtu huru anayestahili kuweka mchango wake katika maendeleo ya taifa.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kwaheri Kaunda, umetuachia suti na Uwanja wa Yanga*



Na Adam Fungamwango

> Dk. Kaunda pia alikuwa mpenzi mkubwa wa soka. Tangu wakati akitawala, timu za soka za Zambia pamoja na timu yao ya taifa zilikuwa na uwezo mkubwa sana. Wakati huo timu ya taifa ya Zambia ilipewa jina la KK 11, ikiwa ni kifupi cha jina lake Kenneth Kuanda......

AFRIKA iliamka na majonzi Alhamisi Juni 17, baada ya kupata taarifa ya kufariki dunia kwa mmoja wa wapigania uhuru wa bara hili na Rais wa Kwanza wa Zambia, Dk. Kenneth Kaunda.

Kaunda alifariki dunia akiwa na miaka 97. Alikuwa ndiye kiongozi wa juu waliokuwa na jukumu la Ukombozi Kusini mwa Afrika, aliyekuwa amebaki duniani.

Alifariki kwenye Hospitali ya Jeshi Lusaka, mji mkuu wa Zambia.

Kiongozi huyo alikuwa rais wa nchi hiyo baada ya kupata uhuru Oktoba 24, 1964 kutoka kwa Waingereza, wakati huo ikiitwa Rhodesia ya Kaskazini. Aliitawala nchini hiyo kwa miaka 27 hadi Novemba 2, 1991 alipoangushwa kwenye uchaguzi.

Kaunda ambaye pia hujulikana kwa jina la utani au a.k.a 'KK', anachukuliwa kama mmoja wa mashujaa wachache walioshiriki kuikomboa Afrika, chini ya Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Hawa walikuwa ndio wazee wa mstari wa mbele kwenye ukombozi kusini mwa Afrika, hasa ikizingatiwa kuwa nchi kama Namibia, Zimbabwe, Afrika Kusini zilikuwa bado hazijawa huru.

Hata hivyo, mwaka 1991, baada ya yeye na chama chake cha UNIP kuangushwa na kuingia madarakani Fredrick Chiluba, kulitokea maasi na kutaka kumpindua rais huyo mwaka 1997. Kutokana na hali hiyo, Chiluba akamtia mbaroni mzee Kaunda, wakati huo akiwa na miaka 73, akimtuhumu kushirikiana na watu waliokuwa wakitaka kumpindua.

Dunia nzima ilishtuka, na rafiki yake kipenzi, Nyerere alilazimika kwenda nchini Zambia na kuokoa jahazi. Alifika nchini humo na kwenda kwenye gereza lililokuwa maeneo ya Kabwe. Nyerere aliingia ndani ya gereza hilo hadi sehemu ambayo Kaunda aliwekwa, akala naye chakula. Akazungumza naye kiasi cha saa mbili hivi na kitu, akatoka. Baada ya muda, Rais Chiluba akatangaza kumfungulia mzee Kaunda.

Dk. Kaunda pia alikuwa mpenzi mkubwa wa soka. Tangu wakati akitawala, timu za soka za Zambia pamoja na timu yao ya taifa zilikuwa na uwezo mkubwa sana. Wakati huo timu ya taifa ya Zambia ilipewa jina la KK 11, ikiwa ni kifupi cha jina lake Kenneth Kuanda, wakiwa na maana ya vijana 11 wa Kaunda.

Klabu ya Yanga ambayo ina historia na Uhuru wa Tanzania, ikaupa jina uwanja wake wa mazoezi ulioko maeneo ya Twiga na Jangwani jina lake. Ukaitwa Uwanja wa Kaunda. Na hii yote ilikuwa kuthamini mchango wa mwanaharakati huyo wa ukombozi na kusaidia nchi nyingi Afrika kupata uhuru, achilia mbali nchi yake.

Pamoja na mafanikio makubwa ya Zambia iliyopata kwenye soka kwa klabu na timu ya taifa, moja ya matukio ambayo hayatosahaulika ni timu ya Mufurilla Wanderers kuchapwa mabao 5-0 kwenye mechi ya Klabu Bingwa Afrika (sasa Ligi ya Mabingwa Afrika) na Simba nchini Zambia, mgeni rasmi akiwa ni Rais Kaunda mwenyewe mwaka 1979.

Baada ya kushinda mabao 4-0 ugenini Dar es Salaam, timu hiyo ilikuwa na uhakika wa kusonga mbele, hivyo kumwita Rais wao.

Akiwa na kitambaa chake cheupe ambacho alikuwa hakiachi popote pale alipokwenda, Kaunda hakuamini kilichokuwa kinatokea uwanjani na viongozi wa Simba waliokuwapo uwanjani siku hiyo, walidai kumsikia akiwauliza baadhi ya viongozi wa chama cha soka Zambia kama wachezaji wa Simba waliocheza siku hiyo ndiyo waliocheza Dar es Salaam au walibadilisha timu. Akaambiwa ndiyo hao hao.

Aliondoka bao la nne lilivyoingia. Wakati anafika Ikulu, bao la tano likatinga na kuiondoa timu yake kwenye Ligi ya Mabingwa.

Ikumbukwe kuwa baada ya Kaunda kuondoka madarakani, ndipo timu ya taifa ya Zambia ikabadilishwa jina na kuwa 'The Mighty Zambia na baadaye Chipolopolo (risasi za moto)'.

Kaunda pia alijulikana kama ndiye mwasisi wa vazi la suti ya Kaunda. Ni aina ya suti ambayo hivi sasa ni maarufu sana nchini.

Hizi ni tofauti na zile za kizungu ambayo ni lazima uvalie na tai.

Aina hii hadi leo huvaliwa na wabunge, maofisa mbalimbali wa serikali na idara zake pamoja na watu binafsi. Ndilo vazi alilokuwa akipenda kulivaa wakati wote akiwa madarakani. Na aina hiyo ya suti ilitokea kupendwa sana na vijana si wa Kitanzania bali dunia nzima na wakaipachika jina la 'kaunda suti.'

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald. Kijana msomi aliyetoka Marekani, anarejea nchini Tanzania. Anakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

BAADAYE tena ikaja meseji nyingine. "Mpenzi nimemtuma kijana mmoja wa bodaboda aje kukuchukua. Ni rafiki yangu na huwa namlipa kwa mwezi kwa mambo ya dharura. Nimekuita ghafla ndiyo maana sitaki uingie gharama, atakuleta salama hadi huku."

Tausi alitaka kupiga simu, lakini wazo likamjia kuwa Donald hatumii simu yake, bali ya rafiki yake mmoja ambaye yuko naye huyo. Anamfahamu mpenzi wake kuwa hana tabia ya kutuma sana meseji, bali kupiga, lakini leo ameamua kutumia zaidi meseji kwa sababu simu siyo yake, hivyo naye akasita kupiga. Akaamua kujiandaa kwenda.

Doroth alikuwa amewasiliana na baba mkwe wake aandike meseji ile kwa sababu ana mtu mwendesha bodaboda ambaye atakwenda kumchukua na kumpeleka wanapotaka.

Baada ya meseji ile, Doroth aliwasiliana na Said. Yule yule ambaye siku za nyuma alimtuma kufuatilia nyendo za Donald hadi akagundua Magomeni Makuti kuna mpenzi wake mwingine Tausi.

Kwa maana hiyo Said hakupata tabu. Alikwenda moja kwa moja hadi kwa kina Tausi na kujitambulisha kuwa ametumwa na Donald kuja kumchukua ampeleke Sinza, kwa maelekezo ya Doroth.


Akiwa amevaa sketi yake ya kisasa fupi yenye mistari myeupe na myeusi iliyoacha mapaja wazi na blauzi nyeupe, akiwa na viatu virefu.

Mwanamke alijipamba akapambika. Alipanda kwenye bodaboda kwa minajiri ya kwenda Sinza kama alivyoitwa na kukutana na mpenzi wake Donald.

Said hakuambiwa lolote kuhusu mpango ule. Lakini alihisi shari. Anakumbuka wiki chache zilizopita alipewa tenda ya kumpeleleza Donald kila anapokwenda hadi alipogundua kuwa huwa anakwenda Magomeni Makuti kwa mpenzi mwingine tofauti na Doroth.

Leo hii anaambiwa amchukue na kumpeleka Sinza. Anayemwambia hivyo ni Doroth aliyempa tenda ya kumchunguza.

Pesa nyingi alizopata alipopewa tenda ile na ambazo amezipata kwa




**Nina maana tutakwambia ukae sehemu fulani, halafu msichana huyo atapita akiwa kwenye bodaboda. Akifika karibu nitakwambia bodaboda inayokuja ndiyo atakuwa amepanda na amevaa nguo fulani, sawa?"**

kumpeleka Tausi Sinza zilimziba mdomo kuhoji chochote.

Akili yake ilimwambia kuwa anampeleka aliko Doroth, maeneo ya Sinza, ili amhoji vizuri kisa cha kumchukua bwana 'ake. Alijua kabisa kuwa huko ni lazima kutakuwa na ugomvi pia.

Binafsi hakutaka kuuona ugomvi huo, aliazimia akifika tu na kumshusha kwenye hoteli iliyotajwa, anageuza na kuondoka haraka. "Watajuana wenyewe, sitaki kuwa shahidi." Alijisemea.

Kutoka Magomeni, alipitia barabara ya Tandale inayokwenda hadi Popo Bawa, Kwa Mtogole na kabla ya kufika kwenye daraja la linalotenganisha Tandale na Sinza, wenyewe wanapaita Manzese Uzuri, simu iliita.

Sauti ilikuwa ni ya Doroth. Maneno aliyokuwa akiuliza, yalimfanya Said kusimamisha bodaboda pembeni na kumuomba radhi Tausi.

"Samahani kuna kitu nanunua dukani mara moja." Aliomba udhuru. Haikuwa hivyo. Alikwenda kujibu swali aliloulizwa na Doroth ambalo halikupaswa kujibiwa mbele yake.

****************************

"Amevaa sketi fupi yenye mistari myeupe na myeusi kama ya pundamilia hivi na blauzi nyeupe." Likuwa ni jibu la Said kwenda kwa Doroth. Hakutaka kulitamka pale mwenyewe Tausi akiwa anasikia kwani ingeweza kumpa mashaka. Ndiyo maana alisimamisha bodaboda na kujifanya anakwenda dukani.

Hata hivyo, kuna swali lilikuja kwenye kichwa chake. Ni kwa nini Doroth alimuuliza nguo alizovaa Tausi wakati akifika tu na kumshusha sehemu waliohidiana atamuona? Na kama hamfahamu vizuri Tausi, yeye ni mtu ambaye Doroth anamfahamu vizuri. Kitendo cha kumuona tu yeye Said anamshusha abiria kingeweza kabisa kujua kuwa anayeshushwa ni Tausi.

"Labda tu alitaka awe na uhakika zaidi." Said hakutaka kuumiza kichwa chake na maswali anayojiuliza ambayo hayana msingi na wala hayamsuhu. Yeye ameshalipwa pesa zake zote, inatosha sana.

Doroth yeye hakuwa Sinza kama ambavyo Said anadhani. Baada ya kumpa kazi hiyo Said anayepaki bodaboda yake Kinondoni kwa Manyanya, alirejea nyumbani kwao Msasani.

Kabla ya kufika huko alimpigia simu mkwewe mtarajiwa mzee Peterson na kumweleza jinsi msichana Tausi alivyovaa.

"Baba, amevaa sketi fupi yenye mistari myeupe na myeusi na blauzi nyeupe."

"Sawa, nimekuelewa mama, ila nitumie tena kwenye meseji ili na mimi nimtumie Bogota."

Doroth alifanya kama alivyoagizwa. Maneno hayo hayo, mzee Peterson aliyatuma kwa njia ya meseji kwenye simu kwa Bogota.

Huyo ndiye yule jamaa aliyepewa kumuondoa Tausi kwenye ulimwengu.

Nia ni kumfanya kijana wake Donald atulie. Arudi kwa msichana waliyemchagulia, Doroth.

Njia pekee walioamua kuitumia ili Donald arudi kwa Doroth ni hiyo tu.

"Nadhani umeipata hiyo meseji."

"Ndiyo bosi nimeipata."

"Wameshavuka kwenye daraja la Manzese Uzuri, kaa tayari." Peterson akamhabarisha Bogota. Wakati huo yeye alikuwa ndani ya hekalu lake analoishi na familia yake Mbezi Beach.

"Mimi sina tatizo, nawasubiria tu."

"Lakini usisahau kama tulivyopanga. Ukimalizana na huyo dada, nataka na huyo dereva naye umshughulikie."

"Pesa iongezwe mzee."

"Wee, nisikilize kwanza, pesa haina tatizo. Ni kwamba awali huyo kijana hakuwa kwenye mipango, lakini naona anaweza kuwa hatari kwako na kwangu kama tukimuacha."

Peterson na Bogota walikuwa wakiongea maneno hayo kwenye simu kwa tahadhari, wakikwepa kutamka maneno halisi kwa kuhofia sauti zao kunaswa mamlaka husika na kuweza kufuatiliwa.

Mpango wa kuondoa uhai wa dereva wa bodaboda aliusuka mwenyewe mzee Peterson kwa kuhofia siri kuvuja. Alihofia kumhusisha mkwewe mtarajiwa Doroth kwa sababu ni mtu wake anayemuamini, hivyo alijua hatoweza kukubali na huenda mpango huo ukavurugika.


"Cha kufanya ni kumalizana kwanza na huyo dada, halafu huyo bodaboda kwanza muache. Atakapotoka hapo mfuatilie na kwenda kumalizana naye sehemu nyingine kabisa, sawa Bogota?"

"Mimi pia nina pikipiki. Nitakula naye sahani moja."

Baada ya kukata, kwenye simu yake hiyo aliangalia saa. Ilimuonyesha kuwa ilitimia tatu kasorobo.

Aliitengeneza bastola yake vizuri kwa ajili ya kuifanya kazi aliyotumwa.

**INAENDELEA JUMAPILI**



# TARAJI KUWA MSEMA CHOCHOTE BET

SHEREHE za 21 za ugawaji wa tuzo za BET zinatarajiwa kufanyika Juni 27, mwaka huu, huku jina la mwigizaji Taraji Penda Henson, limetangazwa kuwa mshereheshaji.

Katika tuzo hiyo ambayo Diamond Platnumz atawania katika kipengele cha mwanamuziki bora wa kimataifa, inatarajiwa kumuona rapa Queen Latifah, akikabidhiwa tuzo ya Lifetime Achievement.

Rapar DaBaby na Megan Thee Stallion, wanaongoza kwa kujitokeza katika vipengele saba, na kuwaacha kwa mbali Cardi B na Drake, ambao wametokea katika vipengele vitano.

## Man Jay Killer anena tuzo BET

MKALI wa muziki wa singeli, Jumanne Chewe maarufu kama Man Jay Killer, akishirikiana na msanii mwenzake Medy Bizy, wametia neno kuhusu vuguvugu linaloendelea kuhusu tuzo kubwa za BET zitakazotolewa June 27, mwaka huu nchini Marekani.

Man Jay, maarufu kama Simba la Singeli, ameliambia BT kuwa ameamua kutumia sanaa ya muziki kuhamasisha jamii kumpigia kura Diamond Platnumz ambaye ni msanii pekee Afrika Mashariki anayewania tuzo hiyo katika kipengele cha Best International Act.

'Kila mtu anaongea lake ila mimi na Medy Bizy tumeingia studio tukatoka na wimbo pamoja na video ya kuhamasisha mashabiki waendelee kumpigia kura Diamond Platnumz ili jamaa ashinde maana akifanikiwa basi limefanikiwa taifa lote, video tayari nimeiachia ipo kwenye chaneli yangu ya YouTube," amesema Man Jay.



## Q Chief aiweka hadharani EP yake

MWANAMUZIKI mkongwe, Q Chief, kesho anatarajia kutambulisha jambo lake na kuwaomba mashabiki wake kuwa tayari kumpokea.

Msanii huyo amesema siku hiyo atazindua EP yake inayoitwa 'Pasi ya Mkaa' ambayo ndani kuna nyimbo tatu kali.

Chilla tayari ameachia cover ya EP hiyo ambayo anasema imegusa maisha halisia ya mtu ambaye amepambana kwa muda mrefu bila kuyumbishwa na changamoto zilizombabili.



# Man United haina mpango na Ramos

**MADRID,** Hispania

MANCHESTER United wameripotiwa kuwa huenda wakajitoa kwenye harakati za kuiwania saini ya beki wa Real madrid Sergio Ramos aliyeachana na wababe hao wa Hispania.

Taarifa ya kuondoka kwa beki huyo mwenye umri wa miaka 35 ilifahamika wiki hii kuwa anaondoka klabuni hapo baada ya mataji 22 katika miaka 16 aliyokaa hapo.

Man United, PSG na Manchester City ni miongoni mwa klabu zilizo kwenye orodha ya kuitaka saini ya beki huyo anayeondoka Real Madrid kama mchezaji huru akiwa amecheza michezo 671 katika miaka 16 tangu ajiunge mwaka 2005 akitokea Sevilla.

Sababu za Man united kusitisha mpango wa kumsajili ni bifu lililokuwepo kati ya kaka yake Ramos, Rene Ramos ambaye hana uhusiano mzuri na Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Ed Woodward.

Sababu nyingine ni kwamba Rene alikwamisha dili la Ramos kutua Man United mwaka 2016.

Man United imekuwa na upungufu mkubwa kwenye eneo lake la ulinzi hali inayosababisha kocha wao, Ole Gunnar Solskjer, kuhitaji kusajili beki wa kati katika dirisha hili na Ramos alionekana kuwa mmoja ya wachezaji ambao huenda wangesajiliwa.

Ramos ambaye alikuwa sehemu muhimu ya mafanikio ya Madrid kwenye kipindi cha hivi karibuni anaondoka kwenye timu hiyo kwa kile kinachoelezwa kwamba hakukuwa na maelewano kati yake na rais wa timu hiyo Florentino Perez.






# GATTUSO KUTUA SPURS

**LONDON,** England

MABOSI wa Tottenham wameamua kumshawishi Gennaro Gattuso aliyekuwa anaifundisha Fiorentina ili awe mbadala wa Jose Mourinho ambaye alifutwa kazi ndani ya kikosi hicho kutokana na mwenendo mbovu.

Timu hiyo imeshtua baada ya awali kuhitaji kumpa dili kocha wa zamani wa Roma, Paulo Fonseca ila dakika za mwisho imeelezwa kuwa wamefungua mazungumzo na Gattuso ambaye anahitaji kusepa katika timu hiyo aliyotumikia kwa muda wa siku 23 akiwa ni kocha mkuu.

Licha ya kwamba Tottenham inataka kumpa dili Gattuso Fonseca alikuwa tayari kujiunga na timu hiyo ambapo walianza mazungumzo na kiongozi wa masuala ya michezo ndani ya timu hiyo, Fabio Paratic kuhusu mpango wake wa kuwa kocha ndani ya kikosi hicho.

Spurs wamesisitiza kwamba suala la fedha halihusiani katika mpango wao wa kubadilisha uamuzi na wameamua kufanya hivyo kwa ajili ya mikakati mikubwa ya timu hiyo.

# Scaloni asifia ushindi Argentina

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

KOCHA Lionel Scaloni amesema Argentina ilikuwa kwenye "kiwango cha kuvutia" wakati walipoibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Uruguay kwenye michuano ya Copa America, juzi.

Lionel Messi alimtengenezea krosi nzuri Guido Rodriguez aliyefunga dakika ya 13 na kuifanya Argentina kupata ushindi wake wa kwanza kwenye michuano hiyo mwaka huu, baada ya mchezo wa kwanza kutoka sare ya 1-1 na Chile.

Scaloni alikuwa akishutumiwa sana baada ya Argentina kutoka sare mechi tatu, akifungana 2-2 na Colombia na 1-1 dhidi ya Chile kwenye kufuzu kombe la Dunia nchini Qatar 2022 mapema mwezi huna.

"Kwa hakika kabisa naamini mchezo wa kwanza pia tulistahili kushinda, lakini kutokana na makosa madogo madogo hatukuweza kufanya hivyo," alisema Scaloni akiwaambia waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo.

"Leo(juzi) tulikuwa na nguvu ya ziada na ndio maana tukapata matokeo tuliyoyahitaji.

"Tulishambulia vizuri na kwa kasi, ingawa timu tuliyokuwa tunacheza nayo ilikuwa ngumu, lakini tulipata ushindi."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KANE ATAJWA PSG

## Wajipanga kumng'oa kule Spurs baada ya Euro 2020, pamoja na...

**LONDON,** England

HARRY Kane yupo tayari kuondoka Tottenham Hotspur ili kutafuta changamoto mpya nje, huku miamba wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Paris Saint-Germain wakiwania saini yake, kwa mujibu wa 90min.

**Kane ameripotiwa kuiambia Tottenham mpango wake wa kutaka kuondoka katika wiki ya mwisho ya msimu huu uliomalizika wa 2020-21.**

Nyota huyo wa kimataifa wa England awali alikuwa akihusishwa na Manchester City, Chelsea na Manchester United.

Tottenham wapo kwenye wakati mgumu wakihaha kutaka kumbakiza nyota wao huyo ambapo wanahofia anaweza kujiunga na wapinzani wao kwenye Liggi Kuu England.

Kwa mujibu wa ripoti, Kane ataweka wazi hatima yake mara baada ya michuano ya Euro 2020 inayoendelea hivi sasa.

Na sasa mtandao wa 90min umebainisha kuwa PSG wamejiweka mguu sawa kuwania saini ya Kane kipindi hiki cha majira ya joto.

PSG ambao msimu uliomalizika walilipoteza taji la Ligi Kuu kwa Lille wapo kwenye mikakati ya kukijenga upya kikosi chao.

Chini ya kocha wa zamani wa Spurs, Mauricio Pochettino, PSG inawinda nyota wakubwa Ulaya ili kujiweka sawa.

Pamoja na Kane, PSG pia wanamuwania nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland na pia wanapambana kumbakiza mkali wao, Kylian Mbappe, ambaye amekuwa akihusishwa na Real Madrid.

## ZISIKUPITE

### HARRY KUMFUATA POCHETTINO

MSHAMBULIAJI wa Tottenham na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, amewaeleza wazi wawakilishi wake kwamba atakuwa tayari kuungana tena na Mauricio Pochettino kule, katika Paris St-Germain. ***(90min)***

### AOUAR AWANIWA ARSENA

ARSENAL watajaribu tena kumsaini kiungo wa klabu ya Lyon Ufaransa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22 na wanajiandaa kumpatia ofa ya mshahara wa pauni 100,000 kila wiki. ***(Sun)***

### PSG YAMTAKA POGBA

PSG watajaribu tena kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28. ***(Le Parisien)***

### TIERNEY KUONGEZA MKATABA

MLINZI wa Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 25, amekubali mkataba mpya na Arsenal ambao atausaini siku chache zijazo. ***(Football.London)***

### RAMOS AWINDWA

SERGIO Ramos analengwa na Manchester United, PSG na Sevilla baada ya mlinzi huyo mwenye umri wa miaka 35 kuondoka Real Madrid. ***(90min)***

### VARENA BADO KUAMUA

MLINZI wa Real Madrid na Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28, bado hajaamua juu ya hatima yake, huku kukiwa na taarifa zinazomhusisha na Manchester United na Chelsea. ***(Goal)***

### MAN WAJITOA KWA TRIPPIER

MANCHESTER United wanaonekana wanaweza kujitoa kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Atletico Madrid na England, Kieran Trippier mwenye umri wa miaka 30, kwa sababu ada yake ni kubwa. ***(ESPN)***

### ISAK AWANIWA CHELSEA

CHELSEA wamejiunga na Arsenal katika mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Real Sociedad na Sweden, Alexander Isak, 21. ***(AS, via Express)***

### RAMSEY KURUDI ARSENAL

KIUNGO wa Juventus, Aaron Ramsey, 30 anaweza kurudi Arsenal. ***(Eurosport)***

### LIVERPOOL YAMTAKA BERARDI

LIVERPOOL ina nia ya kumsajili winga wa Sassuolo na Italia, Domenico Berardi, 26. ***(Gazzetta dello Sport, via Express)***

### LINGARDI KULIPWA ZAIDI

WEST HAM watalazimika kumpa kiungo wa kati wa England, Jesse Lingard, 28, nyongeza kubwa ya malipo ili kumshawishi asisaini mkataba wa kudumu na Manchester United. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

## Mgunda akiri mambo magumu Coastal

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amekiri kuwa walizidiwa uwezo wa wapinzani wao Mbeya City, ndiyo maana wakachapwa mabao 2-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, juzi.

Akizungumza mara baada ya mechi hiyo kumalizika, kocha huyo alisema kuwa mpira umekwisha na wamepoteza, hana kizingizio chochote kwa sababu mechi ilikuwa ngumu na kila timu ilikuwa inahitaji pointi tatu.

"Mpira umekwisha tumepoteza. Tumefungwa na Mbeya City, nimekubali, kiufundi ni kwamba mpira ulikuwa mgumu na kila timu ilihitaji pointi tatu na wenzetu wamefanikiwa kuzipata," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mganda Mathias Lule, amewasifu wachezaji wake kwa kupambana na kuibuka na ushindi kwenye mechi hiyo.

"Tumepata matokeo mazuri, lakini wachezaji wamejitolea sana. Wamecheza kwa maelekezo. Tuliwasoma vizuri Coastal Union tukaona jinsi wanavyocheza tukawaadhibu. Mabao yote tuliyowafunga ni kwa sababu tulifanyia kazi upungufu wao kwa sababu walikuja kwa kuzuia zaidi," alisema Lule.

## Katibu wa Zimamoto afungiwa miaka 2

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya Mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imemfungia kwa muda wa miaka miwili katibu msaidizi wa timu ya Zimamoto, Hassan Muhidini Kipira kutojihusisha na shughuli zozote za soka kwa kosa la kuwafanyia fujo waamuzi.

Akizungumza na gazeti hili, Mjumbe wa Kamati ya Mashindano wa ZFF, Haji Issa Kidali, alisema Kipira aliwafanyia fujo waamuzi waliocheza mchezo wa Juni 17 wakati Zimamoto ikicheza na Kilimani City kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho na Zimamoto ilifungwa 1-0.

Alisema kuwa mbali na kufungiwa miaka miwili, pia atalazimika kulipa faini ya Sh.laki tano Kwa mujibu wa kifungu cha 3 (a) (b) ibara ya 19 ya Kanuni ya mashindano ya msimu huu wa 2020-2021.

Aidha alisema kuwa ZFF kupitia kamati ya mashindano haitasita kuchukua hatua Kwa kiongozi yoyote au mchezaji pale watakapofanya fujo aidha baada ya mchezo au ndani ya mchezo.

"Tunatakiwa kucheza kwa kufuata kanuni na sio kujiamulia kufanya fujo, mpira unaendeshwa na taratibu, hivyo timu ikijiona inaonewa taratibu zipo za kuwasilisha malalamiko katika kamati husika.

Hata hivyo, aliwataka viongozi wa klabu kudhibiti hasira zao badala yake wafuate kanuni na sheria za soka pale wanapoona hawakutendewa haki.

# AZAM FC YAPANGA KUISHUSHA YANGA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC unapiga hesabu ya kushinda mechi zao zilizobaki za Ligi Kuu Tanzania Bara ili kuishusha Yanga katika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo.

Azam ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi 63 baada ya michezo 31 huku Yanga wakiwa na pointi 64 baada michezo 30 wakiwa kwenye nafasi ya pili kwenye msimamo.

Azam juzi ilipata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Gwambina FC na sasa imewapa jeuri ya kuendelea kufanya vizuri katika mechi zijazo.

**Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa Azam, Vivier Bahati, alisema mipango yao ni kupambana kutafuta matokeo chanya katika kila mechi ili kufikia kile kinachotarajiwa.**

Alisema ligi imekuwa ngumu kwa sababu kila timu inahitaji kupata pointi muhimu, wanapambana kufanyia kazi upungufu wao wa kila mechi kutojirudia ili kufikia malengo ya kumaliza kwenye nafasi ya pili ya msimamo.

"Malengo yetu ni kupambana kumaliza katika nafasi ya pili, hatuangalii nafasi kwa sasa inashikiliwa na nani, kikubwa tunaenda kupambana kila mechi kusaka pointi muhimu ili kutuweka katika nafasi ya pili," alisema Vivier.

Alisema baada ya kupata ushindi mnono dhidi ya Gwambina FC, sasa wanaenda kutafuta pointi muhimu katika mechi yao dhidi ya Namungo FC ambayo wanacheza ugenini.



Vijana wa kikundi cha salakasi cha Afro New, wakionyesha manjonjo yao wakati wa maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika yaliofanyika Kigamboni jijini Dar es Salaam jana na kuandaliwa na Baraza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU) (NACOPHA)). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kampira amtetea Metacha*

**Na Adam Fungamwango**

MCHEZAJI wa zamani wa Yanga, Ramadhani Kampira, ameibuka na kumsifu kipa wa Yanga Metcha Mnata kwa kuomba radhi, huku akimtetea kuwa alifanya hivyo kutokana na mhemko na kuchanganyikiwa kutokana na kuzomewa na baadhi ya mashabiki wa Yanga.

Kampira ambaye aliichezea Yanga katikati ya miaka ya 1980, alisema kuwa ameungana na Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi kwa kumtetea kipa huyo.

"Ukiangalia yale mabao yote mawili makosa yalianza kwa mabeki, sasa kwa nini alaumiwe Metacha peke yake. Mimi naungana na mwalimu kumtetea. Mabeki wetu nao wazembe mbona hatuwasemi?" alihoji Kampira.

"Kipa kufungwa ni sehemu ya mchezo. Hakuna kipa yoyote duniani ambaye hafungwi, tena wakati mwingine wanafungwa mabao mepesi kuliko hata ya Metacha. Yule mtoto hajakufuru Mungu, amefanya makosa tu ya kimchezo. Kuna makipa pale Yanga wamefungwa mabao matatu, manne, matano mpaka sita, lakini bado walienḋelea kubaki kudakia Yanga, iweje yeye iwe nongwa?"

Kuhusu kuonyesha ishara ya kuwatusi mashabiki, Kampira alisema ni kweli alifanya kosa, ingawa wakati mwingine kuna watu ambao hawawezi kuhimili kuona watu zaidi ya 30 wanakuzomea.

"Ni kweli klabu kama za Simba na Yanga ni kubwa, unaposhambuliwa hutakiwi kujitetea. Ni lazima utumie busara uvue jezi uingie kwenye gari, ila watu zaidi ya 30 wanakuzomea."

Tayari Metacha ameomba radhi, huku uongozi wa klabu hiyo ukiwa umemsimamisha.

Kwenye mechi iliyochezwa Alhamisi, baadhi ya mashabiki walimzomea kipa huyo licha ya ushindi wa mabao 3-2, Uwanja wa Banjamin Mkapa dhidi ya Ruvu Shooting, kwa madai kuwa alifungwa mabao mepesi kwenye mechi hiyo.

Michezo

Jumapili Juni 20, 2021

Nipashe



Kane sasa atajwa PSG UKURASA 22



Maarcus Rashford (kushoto) wa timu ya England, akiwania mpira na Grant Hanley wa Scotland wakati wa mchezo wa michuano ya Euro 2020 baina ya timu hizo juzi. Mchezo huo ulimalizika kwa suluhu. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yaukaribia ubingwa Ligi Kuu

## ●●● Inahitaji kushinda mechi mbili tu na sare...

**Na Adam Fungamwango**

LUIS Miquissone jana aliipa Simba pointi tatu muhimu na kufikisha jumla ya pointi 70, alipofunga bao pekee kwenye mechi dhidi ya Polisi Tanzania, kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

**Raia huyo wa Msumbiji, alipachika bao pekee dakika 27 kwa mkwaju wa faulo. Ilitokana na beki Shomari Kapombe kukwatuliwa na Juma Ramadhani, pembeni kidogo ya eneo la hatari.**

Ni matokeo ambayo yanaifanya Simba kuendelea kuongoza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa tofauti ya pointi sita, mbele ya watani zao wa jadi Yanga ambao wana pointi 64 mpaka sasa.

Simba ilianza kulishambulia lango la Polisi Tanzania mara tu baada ya pambano kuanza.

Kwa dakika sita za kwanza, lango la maanfande hao lilikuwa kwenye msukosuko, lakini mabeki wazoefu, Kelvin Yondani na Pato Ngonyani walisimama imara kuhakikisha nyavu zao hazitikiswi.

Ilikuwa ni dakika ya saba, Polisi Tanzania ilipopiga hodi kwenye lango la Simba kwa kufanya shambulizi la kushtukiza ambalo nusura lizae bao baada ya Daruweshi Saliboko kuambaa na mpira kwenye wingi ya kulia.

Lakini wakati Tariq Seif anataka kufunga alidhibitiwa na mabeki watatu wa Simba kabla ya kipa Aishi Manula kuuwahi mpira na kuudaka.

Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko, lakini yalionekana kuwasaidia zaidi Polisi Tanzania.

Ni kipindi ambacho Simba ilionekana kupoteana hasa eneo la kiungo na kuwafanya Polisi kutawala wakitandaza kandanda safi.

Dakika ya 64, nusura Hassan Nassor aisawazishie timu yake bao, baada ya kupata pasi akiwa anaangaliana na kipa Manula, lakini alipiga shuti nje.

Nafasi ya wazi zaidi ambayo Polisi wataijutia ilikuwa ni dakika ya 72, baada ya faulo safi iliyopigwa na Kassim Shaaban, mabeki wa Simba walikuwa wazembe kuikoa, ikamkuta Deusededith Cosmas ambaye alipiga kichwa kiliichookolewa kwa ustadi na Manula.

Dakika moja baadaye, Meddie Kagere, aliyeingia kipindi cha pili badala ya Chriss Mugalu aliyeumia, alikosa bao la wazi, alipomegewa pande kutoka kwa nahodha John Bocco.

Simba, yenye pointi 70, inaendelea kukaa kileleni ikiwa imecheza mechi 28, ikihitaji kushinda mechi mbili tu na sare moja ili kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara msimu huu wa 2020/21, ikiwa ni mara ya nne mfululizo, kwani itafikisha pointi 77 ambazo hazitofikiwa na timu yoyote.

Yanga iwapo itashinda mechi zake nne zilizobaki, itafikisha jumla ya pointi 76 tu.

## Ni Yanga vs Mwadui leo

**Na Saada Akida**

TIMU ya Yanga leo Jumapili inashuka kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa kuwavaa Mwadui FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania bara.

Yanga inaingia kwenye mchezo huo ikiwa na kumbukumbu nzuri baada ya kutoka kuifunga Ruvu Shooting mabao 3-2.

Licha ya kuzidiwa alama tatu na vinara Simba, Yanga inaona bado ina nafasi ya kutwaa ubingwa wa Ligi huo msimu huu, huku ikijipanga kushinda mechi zake nne zilizobaki ikianza na mechi ya leo dhidi ya Mwadui FC ambao wako mkiani, kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Yanga wanafundishwa na Kocha Mkuu kutoka Tunisia ambaye ni Nesreddine Nabi huku Mwadui FC ikiwa chini ya Kaimu Kocha Mkuu Fredrick Masombora baada ya kocha mkuu, Amri Said, kuachia ngazi kukinoa kikosi cha timu hiyo.

Timu hizo mbili msimu huu zimekutana mara mbili, katika mechi yao kwanza ya ligi Yanga ilishinda mabao 5-0 na kushinda bao 2-0 tena kwenye wa kombe la Shirikisho.

Kocha wa makipa wa Yanga, Razak Siwa, alisema mapumziko ya wiki mbili waliyopata wakati ligi imesimama kupisha mechi za kirafiki za kimataifa za timu ya Taifa zimesaidia kuwapa maandalizi mazuri na bado wana matumaini ya kutwaa ubingwa.

Alisema wamejiandaa vizuri na amefanyia kazi upungufu wao ikiwemo nafasi ya makipa na kutorudia makosa yaliyojitokeza katika mechi iliyopita dhidi ya Ruvu Shooting.

"Maandalizi yanaendelea vizuri na wamefanyia kazi upungufu wetu ikiwemo kipa, kutakuwa na mabadiliko madogo ndani ya kikosi kwa ikiwemo nafasi tofauti katika mechi zijazo," alisema.

Nahodha msaidizi wa Yanga, Ramadhani Kabwili, alisema malengo yao makubwa ni kufanya vizuri na kusaka heshima kwa klabu hiyo katika kila mechi ikiwamo dhidi ya Mwadui.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >